


SAUTI ISIYOJULIKANA

 ...Yeye ni Uzima wetu, Yote-katika-Yote yetu. Tunakushukuru kwa ajili ya hii, fursa nyingine ya kumkumbatia na kumpenda. Tunakushukuru kwa ajili ya watu Wake, na hapa, usiku wa leo, wamesimama mbele zangu, walionunuliwa kwa Damu Yake, nami nina majaliwa ya kuzungumza nao.

² Ninaomba ya kwamba utaitia mafuta midomo, Bwana, inayonena, masikio yanayosikia, na jalia Neno la Mungu lianguke kwenye udongo mzuri, wenye rutuba wa imani, wengi wapate kuponywa na kuokolewa. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

[Dada mmoja ananena kwa lugha na ndugu fulani anafasiri—Mh.]

³ Amina. Shukrani kwa Baba yetu wa Mbinguni kwa ajili ya faraja hiyo imara kwamba kama tutamwamini, hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya, kuliadini Neno Lake, na kila kitu tunachohitaji kitatolewa. “Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki Yake, mambo mengine mtaongezewa.”

⁴ Sasa, najua labda mumechoka, mimi, asubuhi ya leo tuliwaweka humu jengoni hadi karibu saa tano na nusu, na, huko kwenye kiamshakinywa. Nami nafikiri Ndugu yetu wa thamani David alikuwa na ibada alasiri ya leo, na labda mmejazwa kabisa na *Injili*, jambo pekee liwapasalo kufanya sasa ni kuanza tu kuifuteleza na yote yatakawisha, na kwa hiyo hilo ndilo tunalohitaji.

⁵ Sasa, bila shaka ninashukuru, usiku wa leo, kuwa na kundi hili la wanaume na wanawake waheshimiwa hapa nyuma yangu, ambao ni watumishi wa Kristo, kuniombea wakati nikijaribu kuzungumza nanyi kwa dakika chache. Nami ninawathamini ninyi nyote huko nje mnaomba pia. Kama mkitaka kunifanyia jambo fulani kamwe, niombeeni tu, hiyo ni kweli.

⁶ Unajisikia vizuri zaidi, mwanangu? Itakuwa sawa sasa. Angalia tu, kama kitu fulani hakininii. . .

[Dada mmoja ananena kwa lugha na ndugu mmoja anafasiri—Mh.]

⁷ Amina. Mungu ashukuriwe. Ni ajabu jinsi gani kuketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu! Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kuketi pamoja katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu. Hivi hamuupendi huo? Si ni ya Kimbinguni na ya kupendeza kuwa. . . ?

⁸ Tunasikitika kwamba wengi sana wamesimama nje kwenye kumbi na kadhalika, laiti tungalikuwa na mahali pa kuketi,

bali hatuna, usiku wa leo. Na, labda, kesho alasiri ibada zitaanza, nafikiri ni saa nane. Hiyo ni...? Tisa? Saa tisa, kesho alasiri, samahani. Saa tisa, kesho alasiri, ibada zitaanza, ambayo itawapa nafasi ya kwenda kanisani na kufanya ibada yenu, na kisha mrudi hapa, tufanye ibada zetu kesho alasiri, kisha mrudi kwenye ibada yenu wenyewe.

⁹ Enyi wageni, wachungaji hawa hapa jukwaani bila shaka wangewakaribisha, na karibu na makanisa haya ya Full Gospel. Kama unazuru hapa, hakikisha utampata mmoja wao na u—uende kanisani kesho, kwa sababu hapo ndipo mahali tunapopaswa kuwa, katika nyumba ya Mungu Jumapili, kumwabudu Bwana.

¹⁰ Sasa, halafu kesho alasiri, ninyi mnaokuja kuchukua kadi za maombi, ningependa kuwaalika, hasa sana wachungaji kesho, maana ninataka wanisaidie kuwaombea wagonjwa, Ninataka kuwathibitishia ninyi kwamba Mungu kamwe hajibu maombi ya mtu *mmoja*, Yeye hujibu maombi ya mtu yeyote atakayeomba, na kwa hiyo, waje watusaidie.

¹¹ Nasi tutakuwa tukisambaza kadi za maombi yapata—yapata saa tisa, ama labda kama saa nane na nusu, saa tisa kasorobo, ili kwamba ni—ninii yote, hatutakatiza ibada iliyosalia. Nao hao wavulana watakuwa wakisambaza kadi za maombi yapata saa nane na nusu, kesho alasiri.

¹² Sasa, katika Maandiko, kama tungefungua kwa dakika chache na—na kujaribu kuninii... Asubuhi ya leo, niliikosa tena asubuhi ya leo, ni—nikasema, “Hakika, kama ni saa nne na nusu, mi—mimi...” Nikasema, kwa Billy, “Hebu niangalie nitoke saa tano. Naam,” ama, “niangalie tu, nitapanda kule juu na kusema maneno machache tu.” Nami nikaanza kuzungumza juu ya Bwana, sikutoka nje hadi saa tano na nusu. Kwa hiyo kamwe siwezi kupata ujumbe huo wa dakika thelathini, kwa hiyo nadhani afadhali nikate tamaa na kuacha tu kujaribu.

¹³ Kwa hiyo, basi, katika Wakorintho wa Kwanza katika mlango wa 14, kifungu cha 8, tunasoma hivi:

Maana baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita?

¹⁴ Na sasa, kwa kuwa wengi sana wamesimama, nitajaribu kunena kifupi tu iwezekanavyo. Na nina furaha kusikia taarifa hizi hapa kuhusu, Ndugu, mtu fulani alikuwa akimwambia Ndugu David, kwamba watu mia na *kitu* walimpokea Roho Mtakatifu. Loo, jamani! Hilo si linachoma moyo wako kuwaona tu watu, katika saa hizi za mwisho, wakiingia katika Ufalme wa Mungu, wakimpokea Roho Mtakatifu?

¹⁵ Naye Ndugu yetu David, hapa, ana huduma kwamba yeye huhudumu miongoni mwa makundi ya kikanisa, mnaona, ambayo si ya Kipentekoste. Na—nami nilisoma baadhi ya makala ambayo ni ya kushangaza sana, jinsi ambavyo Mungu

anatembea huko nje, akiwaingiza watu Wake. Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya mambo hayo, kwa ajili ya huduma hizi zote kuu, kumsikia akinena juu ya Oral Roberts, na Tommy Osborn; na hao ndugu kweli ni watoto wa Mungu wa thamani na wapendwa.

¹⁶ Nami nina furaha sana kujua ya kwamba Bwana Yesu aliniruhusu kuwa na sehemu ndogo katika huduma yao, kwa namna fulani kutoa kitu fulani kidogo, ambacho labda katika zile Nchi zingine tutakapoketi chini, nami nione makumi elfu yao yote wakiingia, niseme, “Asante, Bwana. Nina furaha sikujua vema zaidi ya kufanya tu yale uliyoniambia nifanye, na, kwa hiyo, kuwaona wakiingia.”

¹⁷ Sasa, “Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejiweka tayari kwa vita?” Sasa, hilo ni tamshi kwelikweli: *Sauti Isiyojulikana*.

¹⁸ Sasa, kama huna hakika, basi huwezi kuwa na imani. Kama hakuna uhakika, basi huwezi kuwa na imani yoyote, kwa sababu imani ni kitu ambacho ni cha *hakika*, mnajua hilo. Ni—ni, imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Si hadithi ya uwongo, si mawazo tu, wala si tumaini, bali ni *imani*. Nayo imani ni kuwa na hakika, ni kitu ambacho Mungu amekupa. Halafu basi huioni, lakini wewe, hata hivyo u—una hakika tu unayo, kana kwamba ulikuwa nayo moja kwa moja mikononi mwako. Nayo imani ndiyo inayonunua bidhaa unayotarajia.

¹⁹ Na sasa, Paulo akinena hapa juu ya *Sauti Isiyojulikana*. Kwa namna fulani nilichagua hili, kwa sababu, kwa ajili ya ibada ya usiku wa leo, kwa sababu tunaishi katika siku yenye mashaka sana. Kuna mengi sana ambayo hayana uhakika siku hizi. Nasi tunaninii. . . Kama vile taifa letu, usalama wa taifa hauna uhakika sana.

²⁰ Miaka michache iliyopita, mbona, tulisema hakutakuwa na vita tena, lakini tunaona ya kwamba tungali tuna vita. Na tutakuwa navyo mpaka Kristo atakapokuja na kuutwaa ufalme, kwa sababu maadamu Shetani anatawala katika huu ufalme, tutakuwa na vita na matatizo. Lakini kule kutokuwa na hakika ya usalama wa taifa, sio taifa hili tu, bali mataifa yote, kwa sababu mataifa madogo sasa yanaweza, yana silaha zile zile ambazo mataifa makubwa yanazo. Nayo yananinii. . . Usalama bila shaka hauna uhakika. Wala hatujui kwamba *nini*, kuna misukosuko miongoni mwa watu.

²¹ Nikisafiri kutoka taifa hadi taifa, ninaona kwamba kila mtu anaonekana kuwa na wasiwasi. Na wodi za wendawazimu zinajaa, nao watu wananinii, huko chini mtaani, inaonekana kuna wasiwasi mwingi sana, nao wanaharakisha kwa nguvu wawezavyo, mpaka hata hawana adabu, mmoja kwa mwingine. Nami nimeona jambo hilo miongoni mwa watu wote.

²² Hapa hivi majuzi, nilikuwa na mkutano mahali fulani, ambapo palikuwa na uwanja wa kuegeshea magari, nami nikaona miongoni mwa Wapentekoste wetu, wakiyaegesha magari yao kwa upande, *hivi*, kama wangeyaegesha tu kwa mstari, ingempa mtu mwingine nafasi.

²³ Nao wana laana fulani ya Kipentekoste, sijui kama mliwahi kusikia habari zake au la, wanaenda barabarani usiku, ndipo huyo mtu atapunguza taa zake, huyo mtu mwingine hata hatapunguza taa zake (Anaendelea tu, hajali hilo, acha aende.), na kumpofusha kabisa. Hiyo ni laana ya Kipentekoste, mnaona. “Mwache, imempasa . . .” Hatupaswi kufanya hivyo, haidhuru jamaa huyo mwingine anafanya nini, hebu—hebu tuonyesha kilicho ndani yetu. Kama . . . Hebu tupate kitu fulani *hapa* ndani kuonyesha upendo na heshima, na kumheshimu mtu huyo mwingine na—na kumpenda, awe sahihi ama makosani.

²⁴ Kama unaweza tu kuwapenda wale wanaokupenda, mbona, wenye dhambi hufanya jambo lile lile. Lakini sisi ni tofauti, wakati Kristo ameingia moyoni mwetu tunawapenda wale wasiotupenda; tunawapenda wasiopendeka. Nasi tulikuwa hatupendeki wakati mmoja, pia, mwajua, naye Kristo akatupenda mpaka tukamjia. Na basi kama sisi ni wa Kristo na Kristo yuko ndani yetu, tuna Roho yeye yule wa ushirika, na ushirikiano, na kusaidia kujaribu kuusogeza huo mzungu mkubwa, na kuyarahisisha maisha kidogo kwa ajili ya wenzetu.

²⁵ Sasa, hivi majuzi tu nilivutiwa, katika kusoma gazeti, nikiangalia mashindano haya hapa ya makombora. Nami nafikiri kwamba Ndugu duPlessis alitupa somo zuri juu ya jambo hilo asubuhi ya leo, kuhusu ulimwengu kujaribu kumweka mtu angani wapate kuona ni nani anayeweza kufanya jambo hilo kwanza. Sisi tumekuwa na mtu angani kwa miaka elfu mbili: Yesu Kristo. Hiyo ni kweli.

²⁶ Lakini Urusi ilidhani wangeweza kujigamba hivi majuzi walipomchukua mtu, akaingia katika namna fulani ya maskini kifaa kidogo na kuuzunguka ulimwengu katika saa moja ama mbili. Mbona, jamani, Yesu anaweza kuja kutoka Utukufuni upesi kuliko wazo linavyoweza kumfikia huko. Hivyo ndivyo tu, hivi ndivyo *hili* linavyoenda kasi.

²⁷ Mwajua, Einstein alithibitisha ya kwamba kama vitu viwili vyenye nguvu vilikuwa vikija kasi vya kutosha, vingeweza kupita kimoja ndani ya kingine wala kamwe—kamwe visisumbuane. Kama magari mawili yalikuwa yakishuka barabarani, na yote mawili yalikuwa yakienda kwa mwendo wa kasi mno, kasi kuliko sauti, mabilioni tu ya maili kwa sekunde, labda yangepishana moja kwa moja bila kuumizana hata kidogo. Alithibitisha hilo, kwa vitu viwili vyenye nguvu vikigongana.

28 Vema basi, mnaona, sisi ni watu waliojifunga sana na dunia hata karibu yote tunayowazia na tunayoweza kuwazia ni, loo, sisi, wakati na muda na, lakini tunapoondoka katika ulimwengu huu, tunaingia mahali pasipo na wakati. Tunaweza kuwazia maili hamsini kwa saa, maili mia moja kwa saa, maili elfu mbili kwa saa, ama maili elfu kumi kwa saa, hiyo hata haianzi tunapowazia juu ya Umilele, jinsi ilivyo kasi!

29 Yesu, baada ya Yeye kutukuzwa, na kuupokea mwili Wake uliotukuzwa, akafufuka katika wafu, naye alikuwa amepaa Juu kwa Baba, akarudi katika sekunde chache baadaye, na kwa mwendo wa kasi sana, mpaka akaja moja kwa moja mbele ya wanafunzi Wake kupitia kwenye ukuta na hata hakuitikisa ukuta, na hata hivyo akiwa na mwili ambao ungeweza kusimama pale na kula samaki na mkate. Hiyo ni *kasi*, akipitia.

30 Naye anaweza kuja kote kutoka Utukufuni hata moyoni mwako, upesi uwezavyo kumwazia Yeye. Upesi uwezavyo kukiri makosa, Yeye anaweza kumfukuza ibilisi na kujiingiza Mwenyewe ndani, upesi tu uwezavyo kuwa na imani ya kutosha kuliamini. Ni *kasi* jinsi gani!

31 Lakini bila shaka, kama nilivyosema, sisi ni watu wa ardhini, nasi tunaweza tu kupima inchi, maili, na kadhalika, kama vile tu, ilinukuliwa wakati mmoja: Vipi kama mtoto mchanga katika tumbo la uzazi la mama yake angeweza kuwazia? Na ingetokea aseme, “Vema,” wazia, “mnajua, wananiambia bado siku chache tu nami nitazaliwa. Ole wangu! Wananiambia kwamba huko nje, kuna nafasi kubwa sana na kuna jua linalowaka, na watu wanatembea huku na huku. Nitapata riziki yangu wapi? Ninapata riziki yangu mumu humu ndani. Itakuwaje kwangu? Ole wangu nitakapozaliwa!” Vema basi, baada ya yeye kuzaliwa asingetaka kurudi tena.

32 Vema, hivyo ndivyo tunavyojaribu kuwazia, basi zidisha hilo mara mamilioni, kujaribu kulinganisha mambo ya Mbinguni na mambo ya duniani, ni makubwa zaidi. Wakati mauti yanapotupiga, nasi tunaiacha nchi hii nzuri hapa, inayoitwa ulimwengu, tuingie kwenye Nchi ile ng’ambo ya pili, mbona, kamwe tusingependa kurudi mahali hapa tena, nchi hii ya uharibifu na huzuni.

33 Katika jarida la Wafanyabiashara, walichapisha, nitaliita ono, ingawa mimi . . . haikuwa kama ono lolote nililopata kuona; nimeona, Bwana amekuwa mwenye neema kwangu kuniruhusu kuona maono tangu nilipokuwa tu na umri wa chini ya miaka miwili hivi. Halafu basi, ni—nimeona maono mengi, lakini si kama hili, maana nilikuwa nimesimama pale nikijiangalia mwenyewe. Nami nikawaona watu hao, nikawapa mikono, nao walikuwa tu ni *wanadamu* kama sisi tulivyo *wanadamu*, ila tu hakukuwako na jana, hakuna kesho, wala hakukuwako na wazee, wote walikuwa vijana. Na loo, nilifikiri . . .

³⁴ Daima nilitaka kuishi nipate kumwona Yesu akija, kwa sababu kamwe sikutaka kuwa ro—roho, na sikuzote niliogopa mizuka, wala si—si—sikutaka kufa, na kuwa wingu dogo, na kama wingu dogo jeupe likielea mahali fulani, na kuwaona ndugu zangu, niseme, “Hao *hapo*, laiti ningaliweza kuwapa mkono, ila hawana mkono wa kupeana, u—umekufa, na—nao wako kaburini.”

³⁵ Ndipo Maandiko hayo yakafanywa hai, “Nyumba ya maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo nyingine inayongoja.” Loo, kutoka tu hapa moja kwa moja kuingia kwenye hiyo. Loo, nawaambia, hilo linatupa matumaini makubwa. Haidhuru ulimwengu unawazia nini, na jinsi ulimwengu usivyo salama, wakati tunapoweza kuwazia juu ya mambo hayo hofu yote huondoka, kisha tunakuwa raia wenzi wa Ufalme, na kuheshimiana. Na wale ambao si raia wenzetu, tunataka kuwabembeleza wafikie mahali ambapo wanaweza. . . Hakuna mtu anayepaswa kupakosa Mahali hapo.

³⁶ Mimi ni mtu mwenye umri wa makamu, nina umri wa miaka hamsini na miwili, nina mke na mtoto mchanga wanaoketi hapa usiku wa leo, kijana mwanamume, mwanangu hapa, binti wawili nyumbani, na kama haikuwa ni kwa ajili ya kuhubiri Injili na kuwalea hao watoto kuhakikisha kwamba wanakua vizuri, na kwa ajili ya Injili, haingeniogopesha hata kidogo kuondoka sasa hivi, papa hapa mbele zenu. Ni Mahali patukufu! Kwa hiyo mi—mimi. . . Iiondoa hofu yote kutoka kwangu, ambapo wakati mmoja niliogopa kufa, sikuogopi tena; ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo.

³⁷ Sasa, basi vipi kama taifa halina usalama wake? Na vipi kama Urusi ikirusha sputniki, au bomu, ama vyovyote wanavyoyaita hayo makombora? Inaleta tofauti gani? Vema, hiyo ni ngazi tu ya kutupeleka Nyumbani, nji—njia ya haraka tu ya kuepukana na mambo haya yote, kwenda Nyumbani, kwa sababu tutaondoka kabla halijarushwa kwa vyovyote vile.

³⁸ Kwa hiyo, Biblia, ninaamini, inafundisha jambo hilo. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, katika siku za Lutu.” Katika siku za Nuhu, kabla hukumu haijaipiga dunia, Nuhu alikuwa ndani ya safina kabla ya kuwa hata na manyunyuni ya mvua, bila shaka. Hakuwa hatarini. Ndipo yule Malaika akamwambia Lutu, “Hima uende huku, kwa maana siwezi kufanya lolote mpaka utakapotoka hapa.” Mnaona? Iliwabidi waondoke kwanza.

³⁹ Nami ninaamini parapanda ya Mungu italia moja ya asubuhi hizi, waliokufa katika Kristo watafufuka, sisi tulio hai na tuliosalia tutabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, na kunyakuliwa pamoja nao kumlaki Bwana hewani, na ndipo basi ile adhabu kuu ya waovu itaanza duniani.

40 Na kama tunajua tungeweza kulipuliwa vipande-vipande kabla ya asubuhi, na sayansi inasema ni kama dakika moja kabla ya usiku wa manane sasa, Kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia jinsi gani basi? Lakini kutatukia kabla ya mengine kutukia.

41 Kwa hiyo hakuna usalama wa taifa, wasiwasi, watu wakijaribu kutia sahihi mikataba, na kama kundi la watoto, huku wanazozana na kuchomana visu. Nasi tunapaswa kuangalia mambo hayo, kwa sababu ni muhimu kwamba tuyaangalie.

42 Hapa hivi majuzi, makongamano haya ambayo wamekuwa wakifanya, kulikuwako na Bw. Eisenhower na—na Khrushchev waliokutana hapa Marekani. Eisenhower alikuwa, aliwakilisha mataifa yote ya magharibi, naye Khrushchev aliwakilisha mataifa yote ya mashariki. Na hivi mliona, hakuna kitu walichoweza kusema ambacho wangekubaliana? Khrushchev alitoa kiatu chake na kukipigisha kwenye dawati na kadhalika. Vema, hivi hamjui hilo linatimiza yale nabii aliyosema hasa? Mnajua *Khrushchev* inamaanisha nini huko Urusi? Inamaanisha “udongo.” Mnajua maana ya *Eisenhower* katika Kiingereza? “Chuma.” Chuma na udongo, mashariki na magharibi, hivyo vidole viwili vikubwa vya ono la Danieli. Tayari tuko mwisho, eni marafiki.

43 Loo, hatuna budi kuwa na mizozo hii baina ya mataifa, “Taifa litaondoka kupigana na taifa, ufalme kupigana na ufalme, fadhaa ya wakati, dhiki kati ya mataifa, bahari ikivuma.” Mbona, u—ulimwengu unaonekana kana kwamba uko katika hali ya wasiwasi.

44 Jambo lingine, kazi zetu, kazi zetu hazina uhakika sana. Nilikuwa nikizungumza na kijana mwanamume, ambaye ndiyo kwanza arudi kutoka jeshini, huko nje ukumbini, akarudi, hakuwa na kazi. Wala hujui siku moja baada ya nyingine, kama mtu fulani ataninii. . . unafikia uzeeni, ndipo mtu fulani anajuzulu asiye akastaafishwa, wanapata kitu dhidi yako, nawe unajikuta nje mtaani, na huku u mzee sana huwezi kupata kazi. Ukiwa umezidi yapata miaka ishirini na mitano, wewe, haisaidii sana kutafuta kazi siku hizi.

45 Kwa hiyo, wananinii tu, mnaona, kuna. . . Mnafikiri mtu atafanya nini akiisha kufikisha umri wa miaka thelathini na mitano, arobaini, iwapo hana njia ya kujipatia riziki. Kwa hiyo, na halafu basi, kama uko kazini, karibu wakati wowote wanaweza kukuondoa tu kwa sababu ya jambo moja dogo na hilo linakufuta kazi, ndipo umekatiliwa mbali basi, kwa hiyo hakuna usalama kazini. Ni ninii. . . Tunajua hilo, hakuna uhakika wake.

46 Hakuna uhakika ni wakati gani mataifa yetu yangeweza kulipuliwa. Miami, Florida, nafikiri, katika mkutano huu ujao wa Wafanyabiashara Wakristo, kuna mtu anayekuja

ambaye atatoka huko Greenland, ambaye aliweka mkono wake kwenye kifyatulio hivi majuzi, angaliuingiza ulimwengu kwenye maangamizi. Naye alikuwa na wasiwasi sana, hakujua la kufanya. Wana bo—bomu, ama kombora kwenye skrini, nao wakawazia, “Urusi iko tayari kuirusha,” kwa hiyo makombora yametandaa kila mahali, yamewekwa papo hapo kwenye kipipa cha baruti ambapo hiki kitu chote kingeweza kulipuliwa wakati wowote.

⁴⁷ Kwa hiyo hakuna usalama. Hakuna njia ya kuliondokea, huwezi kuchimba chini, hayo mabomu yatalipua futi mia moja na hamsini ardhini, kwa umbali wa karibu maili mia moja mraba. Na hayo ni yale tunayojua, na yale tusiyoyajua je? Kila taifa lina mambo yake ya siri wanayoficha, basi nashangaa tu yale tusiyoyajua.

⁴⁸ Ndipo wanazungumza juu ya gwaride hili lote, na kuingia mahali, na—na kupata mahali pa kujikinga na bomu, wakichimba chini ardhini, wataihamishia serikali chini ya handaki fulani. Ingefaa nini? Vema, kama moja ya hayo mabomu ingepiga, nawe ungekuwa futi elfu moja mia tano chini yake, ingevunja kila mfupa mwilini mwako, huo mtikiso ungevunja.

⁴⁹ Hakuna njia ya kujificha hapa chini, kuna njia pekee unayopaswa kuwazia ya kujificha, hiyo ni kupaa *juu*, uyaondokee, na kuna njia moja tu ya kwenda juu. Loo, ninampenda Mtu wetu aliye angani, na—na—napenda jambo hilo, kwa sababu Yeye alisema angetuondoa kwa hilo, tukiondokee kitu hiki. Naam, bwana.

⁵⁰ Hakuna usalama katika ma—mataifa. Unasema, “Nitakimbilia taifa *hili* dogo, taifa *lile* dogo.” Mbona, *yote* yatalipuliwa. Nayo yataninii. . . Hakuna usalama hapa katika taifa hili. Hakuna usalama katika kazi zetu.

⁵¹ Basi angalieni katika siku hizi, kwamba maisha ya nyumbani yamekuwa hali ambayo inapaswa kushughulikiwa. Jamani, unawaona wavulana wadogo wakitoka na kuchukua bunduki na kuwapiga risasi baba na mama wakati wamelala kitandani. Ukosefu wa uaminifu miongoni mwa wanawake na wanaume wetu, mama na baba zetu. Katika miji mingi mikubwa mume na mke hubeba funguo za siri, ama funguo sawa, hasa, wanabadilishana funguo za nyumba yao, kila mmoja anaingia, anakula chakula mahali fulani, na mmoja ana miadi, na huyo mwingine ana miadi. Jamani!

⁵² Hawana adabu tena, hamna heshima nyumbani. Nyumba siku hizi, hatuna nyumba za mtindo wa kale, huenda ikawa, wengi mno hawana, ambapo Biblia imefunguliwa na baba anasoma mlango fulani, nao wanapiga magoti kuizunguka meza na kuomba. Watu wanaingia, wanaketi na kula. Ninii tu,

nimeona, watu wakienda mezani na kuanza kula kwa pupa, na—na kuzembea, kula, kamwe hawaombi baraka.

⁵³ Mwajua, hiyo ninii tu...Simaanishi kufanya hili kama mzaha, ninataka kulisema kwa kutoa hoja. Niliona wakati mmoja, ilikuwa huko nje tulipokuwa tukiishi shambani, ilikuwa, chini kulikuwako, nguruwe, chini ya mtofaa, nayo hayo matofaa yalikuwa yakianguka na kumpiga kichwani, naye akayala hayo matofaa siku nzima, wala kamwe hakuangalia juu kuona mahali yalipokuwa yakitoka. Hiyo ni kweli. Vema, hiyo haihusu tu nguruwe, hutambui mahali chakula hicho kinapotoka, afadhali uangalie juu na kumshukuru Mungu kwa ajili yake, kwa sababu Yeye Ndiye aliyekupa.

⁵⁴ Hatuna tena usalama wa nyumbani. Mwawapeleka watoto wenu shuleni, wanawafundisha nini huko nje? Mara nyingi, mara nyingi sana, wanawafundisha tunatokana na masokwe, vema, hatuamini hilo. La. Na kama mtu si zaidi ya mnyama basi kuleni, kunyweni, na kushangilia. Hilo ndilo linalowafanya vijana wengi sana kuwa wahalifu, hilo ndilo linalosababisha uhalifu mwingi sana, kwa sababu kama watu si zaidi ya mnyama, inawafanya watende kama mnyama.

⁵⁵ Hatuna budi kumwambia yeye ni mwana wa Mungu, aliyezaliwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, naye *ni* mtu wa maana. Hii ni picha hasi, picha, hasi, ikingojea siku moja kusafishwa, nayo mauti ndiyo kitu pekee kinachoweza kuisafisha. Unapokufa kwa nafsi yako, picha mpya huanza upande wa ndani, ndipo hicho Kiumbe kipya, Kristo Yesu, kinaanza kujidhihirisha Chenyewe. Na moja ya siku hizi, Yeye atakuja na kukupokea Kwake, ndipo kitu hicho chote kitabadilishwa, ndipo basi kivuli hiki hasi kitakuwa halisi.

⁵⁶ Tunaona kwamba usalama wa nyumbani hauna uhakika sana. Kijana mwanamume anaweza kutoka, ajipatie mke, msichana, ajitwalie mume, huenda akatenda kama mwungwana na kadhalika, bali ni—hakika ni kubahatisha. Na tunaona kila kitu kikiendelea nyumbani, kila mahali, kikivunjika. Marekani ina talaka nyingi zaidi, nafikiri, kuliko taifa lingine lolote ulimwenguni, ambako tunadhaniwa kuwa na ustaarabu, na kila mwaka tunaona ya kwamba kila mwaka kidogo watu wanaanza kutenda zaidi kama wasiostaarabika. Ungeweza kuwazia wanaume ambao wangeweza kuwaua wanaume, na wanawake, na watoto wadogo, na ati huo ni—ni *ustaarabu*, unavyopaswa kuwa?

⁵⁷ Katika nyakati za kale, wakati mapinduzi yalipopiganiwa, wakati, ninaamini ilikuwa, Stonewall Jackson, juu ya Mlima Lookout, na jemadari mwingine mashuhuri huko chini, walikuwa wamelengana mizinga, ndipo basi wakati ninii, walipojiandaa kufyatua mizinga kesho yake asubuhi, Jackson

alitoa amri watoke, akawapigia makelele huko chini ya kilima, na kusema, “Ndugu, iweni tayari, tutawarushia makombora.”

⁵⁸ Na sasa huko Ujerumani na mahali mbalimbali, ambapo jamaa kama Hitler, akiwatoa nje maskini hao Wayahudi na, mbona, alama zake zingalipo, waliwaua kwa makumi ya maelfu, kwa mamilioni. Mtu mmoja, wawili, waliwajibika, waliodhaniwa kuwa wastaarabu sana, wenye elimu. Ingekuwa vema kama hatukujua ABC zetu na kumjua Kristo, ndipo basi, isingesababisha upuuzi kama huo.

⁵⁹ La, bila shaka si salama: mambo ya kitaifa, kazi, nyumba. Na sasa ninataka kuzungumza juu ya jambo lingine linalotoa sauti isiyojulikana, kile tunachokiamini sana, tunafanya ubishi mwingi sana kukihusu, hicho ni siasa.

⁶⁰ Majirani wa kale wanakosana, wanabishana na kuzozana, juu ya siasa, mmoja ni wa Democrat na huyo mwingine ni wa Republican. Na—naye. . . Mbona, wanazozana na kupigana juu yake, na wakati pande zote mbili zimeoza na ni chafu ziwezavyo kuwa. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo mmoja hawezi kusema huyo mwingine amekosea maana wote wawili wamekosea. Ni kweli kabisa.

⁶¹ Lakini siasa, miaka kadhaa iliyopita, tulipokuwa. . . Ilikezwa kwa mara ya kwanza kuhusu demokrasia, mmoja wa malodi wa Uingereza akasema, “Ni maneno matupi bila matendo.” Kasema, “Hivi karibuni watakuwa wamesimama, wanasiasa, juu ya masanduku ya sabuni, wakitoa hotuba.” Vema, hiyo ni kweli, kweli kabisa, ila hakuwazia juu ya Bunge lake mwenyewe zuri la Malodi, kile kitakacholipata, pia, na la Wabunge.

⁶² Lakini hapo mnaona ya kwamba mambo haya yote hayana budi kufikia mwisho. Ninaamini katika demokrasia, lakini ninaamini ya kwamba demokrasia ni kama tu ilivyokuwa huko Ufaransa, wakati wa Joan wa Arc. Ufaransa ilihitaji mapinduzi, hiyo ni kweli, lakini baada ya wao kufanya mapinduzi, walihitaji mapinduzi kinzani ya kunyosha baadhi ya mambo waliyokuwa wakiyaasi. Nami nafikiri demokrasia ni sahihi lakini baada ya kupata demokrasia, basi tunahitaji kunyoshwa katika demokrasia. Hiyo ni kweli.

⁶³ Nafikiri Kanisa liko sawa, lakini baada ya Kanisa kushinda basi tunahitaji kunyoshwa kidogo Kanisani. Hiyo ni kweli.

⁶⁴ Siasa, hivi majuzi tu. . . Mimi si Mwanademokrasia wala Mrepublikani, mimi ni Mkristo. Kwa hiyo si—sininii. . . nilimpigia kura Mtu mmoja, huyo alikuwa ni Yesu Kristo, Naye aliikubali, nami sina budi kushinda kwa hiyo, basi huyo—huyo Ndiye ninayemtetea, ni kwa ajili Yake.

⁶⁵ Na mama yangu alikuwa ni Mwanademokrasia, loo, jamani, na baba yangu alikuwa Mrepublikani kiasi hicho. Kwa hiyo hapo ninii. . . tulijuta nyumbani. Na kwa hiyo, mmoja angepiga kura

kila wakati kuangamiza kura ya huyo mwingine. La, bwana, kamwe wasingekubali kushindwa.

⁶⁶ Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo, mnaona, ni kama kundi la watoto wanaocheza. Nafikiri wangukuwa wazuri katika kila chama, ama wabaya katika vyama, inategemea tu huyo mtu. Nafikiri hivyo ndivyo ilivyo kuhusu Methodist, Baptisti, au Presbiteri, au Pentekoste, ni huyo mtu mwenyewe aliye kanisani.

⁶⁷ Kama wewe ni Mkatoliki, nawe unategemea kanisa Katoliki kwa ajili ya wokovu, umepotea, na kama wewe ni Mpentekoste na unategemea kanisa la Kipentekoste kwa ajili ya wokovu, umepotea. Lakini kama wewe ni Mkatoliki na—na unamwamini Yesu Kristo, na kumtumaini Yeye, unaokolewa kwa imani yako kwa njia ya neema, jambo lile lile kwa kanisa lingine lolote lile, ni mtu binafsi. Ni ule mfumo, kama nilivyosema, ambao umetupilia mbali udugu, si kanisa lenyewe.

⁶⁸ Sasa, siasa, huwezi kuziamini. Ndio kwanza tufanye uchaguzi uliothibitika kuwa mojawapo ya mambo ya kidanganyifu kuliko yote yaliyowahi kulikumba hili taifa. Kweli. Lakini walifanya nini? Walikuwa na mtambo ati usio na hitilafu hata kidogo, ndipo makachero wa FBI wakalifichua na kutangaza magazetini na kila mahali, ya kwamba hiyo mitambo ilikuwa imekarabatiwa, kwamba kila walipompigia kura Bw. Nixon, iliwabidi kumpigia Kennedy kura wakati uo huo, nao FBI wakalifichua. Je, walifanya lolote kulihusu? La, bwana. Basi ni danganyifu. Hiyo ni kweli.

⁶⁹ Sasa, mtu fulani alisema, “Utapigwa risasi moja ya siku hizi kwa kusema hivyo.” Hapa ndipo mahali pazuri sana nipajuapo pa kufia, wala sijui sababu nzuri zaidi ya kufia.

⁷⁰ Taifa hili limekuwa sana sana kama Israeli. Israeli walikuwa ni watu waliokuwa utumwani. Nalo kundi hilo dogo la Waisraeli, waliokuwa utumwani, nao walipenda uhuru, na walitaka kumwabudu Mungu wa kweli na aliye hai, Mungu aliwakomboa kutoka kwenye mashimo yao ya utumwa na kuwapeleka katika n—nchi waliyoahidiwa, kisha wakawafukuza wenyeji wa nchi hiyo, na kuiteka nchi hiyo na kuwa taifa lenye nguvu, walikuwa na watu wenye nguvu.

⁷¹ Nalo taifa hili lilifanya jambo lile lile: Tulikuwa watu waliofungwa, hatuna uhuru wa dini, ndipo Mungu akawatuma babu zetu kwa taifa hili, tukawafukuza wenyeji na kuiteka, nalo limekuwa taifa linaloongoza ulimwenguni.

⁷² Nayu Israeli ilikuwa taifa linaloongoza ulimwenguni katika siku zake, kwa sababu walikuwa na watu wakuu, watauwa, watu kama Daudi, kama Sulemani, watu wenye heshima, watu waadilifu, watu waliomjua Mungu na kumtumainia Mungu. Lakini siku moja, akaja haini aliyechaguliwa kwenye kiti cha enzi, na huyo alikuwa ni Ahabu, mwaminio mkwamia mpakani.

⁷³ Hili taifa lilijulikana kote ulimwenguni kama taifa linaloongoza, maana tulikuwa na watu watauwa nyuma yake: Abraham Lincoln, George Washington, watu kama hao waliomtumainia Mungu, na kumcha Mungu. Lakini kama tu vile Israeli ilivyofanya kosa lake na kumwingiza Ahabu ndani, sisi tulifanya jambo lile lile si muda mrefu uliopita.

⁷⁴ Wakati Ahabu alipoingia, alimwoa Yezebeli, naye Yezebeli alikuwa kafiri. Wala haikuwa Ahabu, Ahabu alikuwa ni jamaa mzuri sana, alitaka kuninii. . . alitubu mara nyingi, bali haikuwa Ahabu, ilikuwa ni Yezebeli nyuma ya kiti cha enzi, maana alikuwa amemwoa, naye akamtawala na kuleta dhambi kwa taifa, na dhambi kwa watu.

⁷⁵ Na jambo lile lile limetukia sasa. Baadhi yenu ninyi Wanademokrasia wazuri, wenye msimamo thabiti huenda msikubaliane na hilo, lakini hebu niwaambie, mliwaza sana juu ya siasa zenu badala ya Biblia ya Mungu, mkaziacha ziingie moja kwa moja, zichukue mamlaka. Mungu kwanza! Tuko hapa kwa ajili ya uhuru wa dini, wa *nini*? Mfumo huo wa Yezebeli. Rais wetu sasa ameolewa na mfumo huo wa Yezebeli. Ni kweli kabisa. Kama tu ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa. Si yeye ambaye mimi. . . Bw., Rais, sina neno dhidi yake, ila mfumo huo ulio nyuma yake!

⁷⁶ Mliona hivi majuzi tu kuhusu shule? Jinsi walivyojaribu kuzichukua hizo? Bila shaka. Huo ni mwanzo tu wake, ngojeni tu, naam, bwana, ngojeni tu. Mmeonywa vizuri kuliko hivyo na wahubiri wa Roho Mtakatifu ambao wamewaonya. Lakini kuna nini? Tuliuzua haki zetu za mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya siasa.

⁷⁷ Mlifanya siasa kanisani, na kadhalika, halafu mlifanya nini? Mmetia nanga taifa zima na kuuza haki zenu za mzaliwa wa kwanza mlizopewa na Mungu kwenye kitu kile kile kilichowaleta hapa, mpate uhuru. Hiyo ni kweli kabisa. Amina. Sikukusudia kuingilia jambo hilo. Imechelewa sana sasa, hiyo ni kutimiza unabii, hiyo ndiyo sababu hasa wasingelisahihisha baada ya hiyo mitambo kuthibitishwa kwamba imekarabatiwa. Hii imechelewa kuliko mnavyodhania, haina budi tu kuwa.

⁷⁸ Sasa, hapana hatuwezi. . . Siasa hizi zinatoa sauti isiyojulikana. Hujui. . . Unaweza kupiga kura, na kupiga kura, na kupiga kura, na kupiga kura, haileti tofauti yoyote, wanaiendesha watakavyo. Kwa hiyo kuna mashaka katika siasa.

⁷⁹ Kanisani kuna mashaka. Loo, tuna mamia ya madhehebu, kila moja likisema, "Letu ni la kweli. Wao hawafai chochote. Tunalo." Yapata madhehebu mia tisa mbalimbali hapa Marekani, *yote* yanawezaje kuwa sahihi? Sasa, kuna sauti isiyojulikana hapo mahali fulani. Haisikiki sawa.

⁸⁰ Mmoja anasema, "Wewe njoo ukajiunge na kanisa letu, na uliache *hili* uje, ukajiunge na letu." Anayefuata anajiunga na ninii yao. . . Watu hubeba barua kutoka kanisa hadi kanisa

mpaka wanaichakaza, wakibadilisha tu jina, kutoka Methodisti, likawa Baptisti, likawa Presbiteri, likawa Lutheri, likawa Pentekoste, Umoja, Uwili, Utatu, na kwa nini ni . . . Jamani! Kwa nini usisahau jambo hilo? Andika jina lako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo Mbinguni, haitakubidi kulihamisha tena. Hiyo ni kweli.

⁸¹ Kutokuwa na uhakika, kanisa likitoa sauti zisizojulikana. Wabaptisti walikuwa na msemo si muda mrefu uliopita, “Milioni moja zaidi katika mwaka wa ’44.” Tulipata nini? Mlipata wanaojiunga milioni moja zaidi, bila shaka.

⁸² Ikiwa watu wote walio katika Marekani hii wanaokiri kuwa Wakristo katika kitengo fulani, Katoliki au Protestanti, wa makanisa, kama kila mmoja wa watu hao angalikuwa ni Wakristo waliozaliwa mara ya pili, ninawaambia, nchi hii ingekuwa kavu sana, mwuza pombe haramu angelazimika kujikakamua apate unyevu wa kutosha kutema mate. Hiyo ni kweli. Ingekuwa, loo, ingekuwa ni tofauti! Lakini siku hizi wanawauzia watu hao wiski kisha wanawakamata kwa kunywa pombe. Ee Mungu, uturehemu! Siasa, kanisa, na kila kitu bila shaka ni sauti isiyojulikana, havina uhakika.

⁸³ “Njoo ujiunge, njoo uandikishe jina lako,” hilo silo wazo. Njoo ukazaliwe, njoo ukafe, njoo na uoze kwa nafsi yako na mawazo yako mwenyewe na umruhusu Kristo aingie, ndipo uwe kiumbe kipya; hilo ndilo wazo.

⁸⁴ Kutokuwa na uhakika kitaifa, kutokuwa na uhakika kazini, kutokuwa na uhakika nyumbani, mashaka yanavuma katika siasa, sauti zisizojulikana makanisani. Vema, hata maisha yenyewe hayana uhakika. Hatujui tunaondoka lini, lakini kuna jambo moja la hakika, tunajua hatuna budi kuondoka.

⁸⁵ Kama vile msemo wa kale ulivyo, “Kuna mambo mawili ambayo ni ya hakika, hayo ni kodi na mauti.” Nawe utakutana na yote mawili, kwa hiyo kwa nini usijitayarisha kwa ajili yake? Hiyo ni kweli.

⁸⁶ Mashaka ya maisha, mashaka ya kanisa, mashaka mengi sana. Ndipo unasema, “Ndugu Branham, hakika unatuhangaisha. Kuna chochote cha hakika?” Ningeweza kusimama hapa na kusoma orodha ya mambo, hapa, ambayo hayana uhakika. Taifa halina uhakika, sauti isiyojulikana, ni nani ajuaye la kufanya? Kazi, siasa hazina uhakika, kanisa halina uhakika, maisha ya nyumbani hayana uhakika. Ni nini cha hakika? Kuna chochote kilicho hakika? Naam, kuna Kitu kimoja nitakachowahakikishia ni cha hakika, hicho ni Neno la Mungu. Hiyo ni kweli.

⁸⁷ Katika Mathayo mlango wa 24 na kifungu cha 35, Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe.” Kwa hakika tu kama vile Mungu anavyosema jambo lolote, ni hakika vivyo *hivyo* tu litatimia.

⁸⁸ Kabla hakujakuwako na ulimwengu, kabla hakujakuwako, miaka elfu nne kabla Kristo hajazaliwa, Biblia ilisema Yeye alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kwa kuwa wakati mpango wa Mungu ulipochorwa, basi alijua yatakayotukia, katika akili Yake kuu alijua ya kwamba ingembidi kumwua Mwanawe Mwenyewe apate kuuokoa ulimwengu, nalo lilitatuliwa mara tu Mungu alipolinena. Amina.

⁸⁹ Mungu anaposema jambo lolote, ni la Milele tu kama Yeye alivyo; haliwezi kushindwa, Neno la Mungu. Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe.” Loo, bila shaka ni la hakika, hakuna mashaka juu Yake.

⁹⁰ Huenda ikakufanya utende mambo ya kigeni unapolipokea, huenda usitende kama ulivyokuwa ukitenda, na hilo ni jambo moja la hakika, pia. Paulo alisema, “Maisha ninayoishi sasa,” hapana shaka aliishi maisha tofauti wakati mmoja, na hata hivyo alilelewa kidini, bali alikuwa na aina mpya ya Maisha, “si mimi, bali Kristo aishiye ndani yangu.” Mnaona, alikuwa amepita kutoka kwenye maisha mamoja kuingia katika Mengine. Na kwa hakika tu kadiri unavyolipokea Neno la Mungu moyoni mwako, basi utakuwa na Uzima wa Milele nawe utatenda kigeni, uonekane wa kigeni, na uwe tofauti na vile ulivyokuwa.

⁹¹ Hebu na turudi tu nyuma kwa dakika chache sasa, kama dakika kumi, na tuangalie baadhi yao ambao wameninii, watu katika nyakati zilizopita, ambao wametulia tu juu ya uhakika wa kutangazwa kwa Neno la Mungu.

⁹² Nuhu, huko nyuma kabisa hapo mwanzo, katika . . . kabla ya yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika, labda mkulima huko nje kondeni, lakini siku moja alikutana na Mungu. Ndipo Mungu akamwambia itanyesha. Nuhu alikuwa na hakika tu mvua itanyesha kadiri—kadiri alivyokuwa na hakika yeye alikuwa ni Nuhu. Naye akaanza kuitengeneza safina kwa ajili ya kuiokoa nyumba yake, kwa sababu alikuwa na hakika kwamba itanyesha.

⁹³ Haidhuru ilionekana isiyo ya kisayansi jinsi gani, haidhuru ni *sayansi* ngapi zingeweza kumthibitishia hakuna hata chembe moja ya maji huko juu, kusingekuwako na mfano wa wingu, kusingekuwako na *hiki, kile*, ama *kinginecho*, haidhuru ilionekana ya kisayansi jinsi gani, alikuwa na hakika itanyesha, naye akajiandaa kwa ajili yake. Amina. Hivyo ndivyo, ndugu, unapokuwa na hakika, fanya maandalizi kwa ajili yake.

⁹⁴ Kama una hakika, usiku wa leo, kwamba hutaondoka hapa ukiwa mgonjwa, kama Mungu amekufunulia, hutatoka, fanya maandalizi. Kama ukisema, “Mimi ni kiwete, si—si—siwezi kutembea, bali nina hakika moyoni mwangu, Mungu alinena nami muda mfupi uliopita na kusema, ‘Usiku wa leo utatembea ukitoka kwenye jengo hili,’” jitayarisha tu, utaondoka. Hiyo

ni kweli. Uwe na hakika moyoni mwako. Mungu anaponea, ni hakika, ni hakika Milele wakati Mungu anaponea, hakuna sauti isiyojulikana hapo, hata kidogo.

⁹⁵ Musa, mtu aliyekuwa mwerevu, mwenye elimu ya juu, msomi hodari, angeweza hata kuwafundisha Wamisri, alikuwa mwanajeshi, tunaambiwa, alijua ustadi wote wa—wa uanajeshi, ndipo akagundua kwamba alishindwa katika uanajeshi wake, wakati alikuwa na jeshi lote la—la Farao nyuma yake, naye angekuwa mrithi wa kiti cha enzi.

⁹⁶ Lakini siku moja, baada ya kukimbia na kuwa huko nje nyikani kwa miaka arobaini, ameo, akatulia, alikuwa na mke na mtoto, siku moja upande wa nyuma ya jangwa, mzee, mwenye umri wa miaka themanini, akiwa na masharubu marefu, akiwachunga kondoo, alipata kuona kichaka kilichowaka moto, akasimama mbele ya kile kichaka na kumsikia Mungu akisema, “Hakika, nitakuwa pamoja nawe, shuka uende Misri.” Naye Musa alikuwa na hakika ya kwamba hakuna kitu kitakachomsumbua. Alijua ya kwamba alikuwa akishuka kwenda kuwakomboa watu, kwa sababu alikuwa na hakika Mungu alimwambia ukweli, kwa sababu alijua ilikuwa ni Mungu, naye alijua ilikuwa ni mpango wa Mungu na Neno la Mungu kuwakomboa.

⁹⁷ Sasa, kama Musa angeweza kuwa na hakika hivyo, kwa mzee mmoja kushuka kwenda na kulitoa taifa moja kutoka katika taifa lingine, tunapaswa kuwa na hakika zaidi jinsi gani tunaposoma Neno la Mungu na kuona ya kwamba haya, tunaishi katika wakati huu tunaishi sasa, tunapaswa kuwa na hakika sana kuhusu uamsho ujao, inatupasa kuwa na hakika sana kuhusu kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, tunapaswa kuwa na hakika sana kuhusu uponyaji wetu, Mungu alisema hivyo, hilo latosha.

⁹⁸ Musa alikuwa na hakika kabisa ya kwamba Israeli itakombolewa, hakujuu vipi, hakuwa na chochote mkononi mwake ila fimbo kuukuu, bali alikuwa akishuka kwenda kwa vyovyote vile. Hakujuu jinsi jambo hilo lingekuwa, bali alijua ya kwamba Mungu alikuwa amesema naye naye alikuwa njiani, angeshuka kwenda kule na kumwacha Mungu afanye alichotaka baada ya yeye kufika kule. Kwa hiyo hiyo ndiyo njia.

⁹⁹ Unasema, “Ndugu Branham, nina kansa. Ninaweza kuwa na hakika?” Acha Mungu aseme nawe, likubali Neno. “Vema, daktari alisema . . .” Najua huyo mtu amefanya yote aliyoweza kukufanyia, hapana shaka, lakini kama Mungu amesema nawe, kuwa tu na uhakika kwamba ni Mungu na kisha uendelee.

¹⁰⁰ Mungu anasema nawe, unamwona Mungu, unaona nguvu Zake, unaona kufufuka Kwake, unaona kazi Zake, na ishara Zake, nawe unajua ya kwamba Yeye yupo hapa, basi mkubali na ulikubali Neno Lake. Kama unaweza kulihisi huko chini kabisa

moyoni mwako kwamba ni kweli, basi endelea tu moja kwa moja, ufanye maandalizi kwa sababu kila kitu kitakuwa sawa.

¹⁰¹ Maskini msichana huyo, niliyenena habari zake hapa, hivi majuzi usiku, labda maskini msichana huyo yuko hapa usiku wa leo, mwenye yule mtoto mchanga aliyekuwa na mguu huo ulioning'inia, kutoka Zion, alikuwa na hakika sana kwamba mtoto huyo mchanga angetembea, akamnunulia jozi ya viatu, mnaona, kisha akashuka apate kuombewa.

¹⁰² Ndipo alipovuka jukwaa kuombewa, aliangalia na mtoto huyo mchanga akajaribu mguu wake, wala haukupata nafuu, kwa hiyo akashuka akaenda kwa Mama, naye Mama alijua nilikuwa huko nje ofisini, kwa hiyo akamtuma huyo msichana huko nje. Huyo msichana mdogo akaingia, nami nikasema, "Hivi wewe si ndiye yule mama aliyeombewa jana usiku?"

¹⁰³ Akasema, "Naam." Kasema, "Lakini, unajua, Bwana amenena nami, na kuniambia nimlete mtoto wangu mchanga kwako, nawe ukiweka mikono yako juu ya mtoto wangu, atatembea."

Nikasema, "Vema, basi hilo—hilo tu ndilo linalohitajika. Mungu alisema hivyo, hi—hi—hilo tu ndilo unalopaswa kufanya. Liamini tu."

Kasema, "Lakini huyu mtoto mchanga hatembei."

Nikasema, "Hilo halina uhusiano wowote nalo. Kama una hakika, hutakuwa ukilipigia swali."

¹⁰⁴ Kwa hiyo tukaomba na kumwekea mikono huyo mtoto mchanga, nami nikasema, "Dada, ningeweza kusimama na kufanya hivyo siku nzima sasa, kama una hakika na kweli unaamini, litatukia, bila shaka itakuwa hivyo."

¹⁰⁵ Ndipo alipoanza kutoka, alitaka kunisikia nikisema jambo lingine. Maskini jamaa mdogo, maskini mama, natumaini. . . Huenda yeye. . . Uko hapa usiku wa leo, Dada, kutoka Zion, uliyekuwa na mtoto huyo hapa hivi majuzi usiku? Uko humu jengoni? Inua mkono wako iwapo upo. Nilikuwa. . . Yeye alikuwa. . .

Baadhi yenu mlikuwa hapa hivi majuzi usiku wakati alipokuwa hapa. Kuna mtu yeyote aliye hapa aliyekuwako, wakati alipokuwa hapa hivi majuzi usiku? Naam, sisi. . . Vema.

¹⁰⁶ Sasa, alikuwa na hakika ya kwamba Bwana atamponya mtoto huyo mchanga, bali alitaka niseme jambo fulani kulihusu. Vema, tayari nilikuwa nimewaambia hao ndugu pale nilikuwa nimemwona mtoto huyo yuko sawa, bali nilitaka tu kuona kile atakachofanya juu yake.

¹⁰⁷ Kwa hiyo wakati alipotoka chumbani, kidogo amevunjika moyo, kidogo akilia, aliangalia nyuma, maskini mume wake akatoka nje, kwa hiyo basi alipoangalia nyuma akasema, "Kasisi Branham?"

Nami nikasema, “Naam, mama.”

Akasema, “Je, ni mapenzi ya Mungu kwa mtoto wangu kuwa mlemavu?” Alitaka tu kusikia kile nitakachosema, akalivuta moja kwa moja.

Nikasema, “La, mama, sivyo.”

Akasema, “Asante, bwana.” Huyo akatoka mlangoni.

¹⁰⁸ Ndipo yapata juma moja baadaye, mguu wa huyo mtoto mchanga ukanyoka, kawaida na mzima. Mnaona? Mnaona, lishikilie tu, shikilia kitu *fulani*, lishikilie. Hakika! Naam, bwana.

¹⁰⁹ Musa alikuwa na hakika ya kwamba Mungu atawakomboa Israeli.

¹¹⁰ Eliya, juu ya kilele cha mlima, katika siku zile alipodhani alikuwa ndiye pekee aliyesalia, Mungu alikuwa amempeleka kule juu na kumlisha kwa kunguru, na kumdumisha hai mpaka alipoweza kutimiza unabii wake, Yeye alimwondoa tu uwanjani. Huko chini katika siku za Ahabu, jamaa wote walijisalimisha, bali walikuwa na maskini jamaa mmoja kule chini, asingejisalimisha, huyo alikuwa ni Eliya, bado alimwambia Yezebeli ilikuwa ni kosa kwake kutenda hivyo. Haidhuru hao wengine walifanya nini, papo hapo aliwakemea vikali alivyoweza.

¹¹¹ Siku moja Mungu akasema, “Sasa, ulitabiri vya kutosha dhidi yao, njoo utoke hudumani, nami nitaachilia hukumu za unabii wako ziwashukie.” Kwa hiyo Eliya akapanda juu ya mlima, huko juu kwa muda wa miaka mitatu na nusu, ama, miaka mitatu, wakati wote walipokuwa ni kuguguna ndimi zao kwa maumivu, ila yeye alikuwa ameketi kando ya kijito kidogo, chemchemi ndogo, alikuwa na ufunuo wa kiroho wakati wote, maji ya uzima yakibubujika. Hao wengine . . .

¹¹² Basi sikilizeni, ndugu, dada, hebu niwaambie, moja ya siku hizi wakati Mungu anapotosheka tu na jambo hili hapa, Naye atawaondoa wote walio wa kweli hudumani na ndipo mtataka uamsho. Halina budi kutimia, nabii alisema kutakuwa na wakati katika siku za mwisho, wakati kusingekuwako na njaa ya chakula na maji tu, bali ya kusikia Neno la Mungu. Basi watumishi wa kweli wataondolewa, ndipo kutakuwa na njaa katika siku za mwisho, hakika itakuwako.

¹¹³ Sasa, angalieni, lakini Mungu akamwambia basi kuhusu ni kwa nini Yeye alimtoa mafichoni mwake kule juu, akasema, “Nenda, ukamwite Ahabu, ukamlete juu ya mlima.” Ndipo basi wakati Eliya alipokuwa na hakika sana ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu aliyemwambia kufanya hivyo, hata akawaita makuhani mia nne, nao wakamleta fahali, na kuomba siku nzima, wakati Eliya akitembea huku na huku akiwadhihaki.

114 Akasema, “Kwa nini msipige makelele zaidi kidogo, labda ana shughuli, labda amelala, ama hataki kusumbuliwa, ama kitu fulani.” Kasema, “Mwiteni kwa sauti kubwa zaidi.” Nao wakamdhihaki tu, wakati walipokuwa . . . Kwa nini? Kwa sababu alikuwa na hakika. Alijua hakukuwa na nguvu katika sanamu hiyo, naye alikuwa na hakika kwamba alikuwa akiwasiliana na Mungu aliye hai.

115 Hiyo ndiyo sababu usiku wa leo, ndugu, ninalisema kwa upendo na heshima, ninajua hakuna uamsho katika umadhehebu, bali ninajua kuna Mungu aliye hai ambaye ana uamsho, hebu tuurudie huo. Nina hakika nalo, nina hakika nalo, ninajua ya kwamba ni kweli. Mungu kamwe hatafanya hivyo, hakuna mahali walipowahi kuinuka wala kamwe hawatainuka. Lakini Mungu atachukua watu kutoka kwa watu hao kwa ajili ya Jina Lake, Yeye atafanya hivyo.

116 Kwa hiyo Eliya wakati alipoweka hayo, hayo mawe kumi na mawili kule juu, kisha akamweka huyo fahali na kumchinja na jinsi hasa Mungu alivyomwambia, alikuwa na hakika tu ya kwamba Moto huo ungeshuka kadiri alivyokuwa na hakika kwamba alikuwa ni Eliya.

117 Hakuna kitu, hakuna Moto huko juu, wala hakukuwa na maji huko juu, haikuwa imenyeshwa kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita. Naye akatoka huko nje akiwa mtulivu na mnyamavu, kwa sababu alikuwa na hakika. Haikumbidi kusema, “Sasa, ndugu, nitatoka niende nikajaribu. Ni—nitaona. . .” La, la. Ile Sauti ilikuwa imenena na Eliya, Eliya alikuwa na hakika ilikuwa ni Mungu. Amina. Unapokuwa na hakika ya kwamba ni Mungu, jambo fulani halina budi kutukia.

118 Eliya alitoka akaenda pale na kusema, “Ee Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa Israeli,” mnaona, kamwe hakumwita jina lake la mdanganyifu, Yakobo, alimwita jina lake la mtawala, Israeli, “Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Israeli, na ijulikane leo ya kwamba Wewe ni Mungu na mimi ni nabii Wako.” Na yapata wakati huo Moto ukaanza kushuka. Kwa nini? Alikuwa na hakika utashuka. Akasema, “Nimefanya haya yote kwa amri Yako.”

119 Wakati ukiwa na hakika ya jambo lolote! Kuna Sauti moja ambayo unaweza kuwa na hakika nayo, na hiyo ni Sauti ya Mungu. Neno la Mungu ni la hakika.

120 Daudi, alikuwa amemjaribu Mungu. Siku moja alipokuwa akichunga kondoo, dubu aliingia na kumchukua mmoja wao, akachukua kombeo dogo na kumwangusha dubu huyo chini. Sasa, mnajua jiwe dogo katika kombeo halitamwangusha dubu. Ndipo huyu hapa simba mkali anakuja, akamnyakua nanii, mmoja wa hao jamaa wadogo na kukimbia naye. Daudi akamfuatilia, akimtumainia Bwana, naye akatupa jiwe hilo na kumwangusha simba chini, akamwua huyo simba.

121 Ndipo siku moja alikuwa amesimama pale na kumwona Mfilisti asiyetahiriwa akisimama akisema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama upuuzi huu.”

122 Ndipo maskini Daudi, labda ameinama mabegani mwake, na kadhalika, akasema, “Mnataka kusema ya kwamba mtasimama hapo na kumwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa ayatukane majeshi ya Mungu aliye hai?” Akasema, “Nitaenda kupigana naye.”

123 Na jamani, wakati yeye, Sauli alipojaribu kuweka Ph.D. ya—yake juu yake, mbona, haikumkaa hata kidogo. Hakujuu lolote kuhusu jinsi ya kusema, “*Amina*,” sawa tu, mwajua, na kadhalika. Naye akasema, “Sijui lolote kuhusu upuuzi huo, sijui lolote kuhusu huo, bali nina kitu ambacho nimekiamini. Sijui Mungu atanifanyia nini kwa Ph.D., bali ninajua Yeye—Yeye amenifanyia jambo hili,” kisha akasema, “Mungu Yule aliyenwezesha kumwua simba kwa kombeo hili, Mungu Yule aliyenijalia kumwua dubu kwa kombeo hili, ni zaidi sana vipi,” amina, “ni zaidi sana vipi Yeye atamkabidhi Mfilisti huyo asiyetahiriwa mikononi mwangu!”

124 Wanaume kwa wanawake, marafiki, mnatambua Mungu wa Mbinguni aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu, Yeye hajafa bali yu hai? Na kama Yeye alilitimiza Neno Lake kwa Daudi, kama alilitimiza kwa Eliya, kama alilitimiza kwa Musa, kama alilitimiza kwa wana wa Kiebrania, kama alilitimiza kwa Danieli, Yeye atalitimiza kwa ajili yangu na yako, kama tuna hakika kwamba ni Mungu. Haleluya! Jamani, ninajisikia kubarikiwa sasa hivi. Naam, bwana.

125 Nilijua usiku huo. . . Mtu fulani alisema, “Ndugu Branham, hivi huogopi kosa?” Ati kosa? Mungu anawezaje kufanya kosa? Bila shaka. Malaika huyo alikuja pale usiku huo na kusema alikuwa akinituma kufanya jambo fulani hili, kuhusu maono, na kadhalika. Ulimwenguni kote nimeenda nayo, pamoja na watu wa kila namna na mahali pa kila namna, wala hayakushindwa hata wakati mmoja. Kwa nini? Nina hakika ilikuwa ni Mungu. Ilikuwa kulingana na Neno Lake, ni kulingana na Roho Wake, ni kulingana na tabia Yake, na iko kwenye wakati unaofaa kabisa kwa Uzao wa Ibrahimu.

126 Ninaweza kuona ni kwa nini makanisa ya kawaida hayataupokea; wala Malaika huyo hakushuka na kumhubiria Lutu na hao wengine, Yeye alikaa pamoja na Wateule. Walikuwa na mmoja wa kushuka kwenda kule na kulihubiria kundi hilo huko chini.

127 Na hiyo ndiyo sababu wa—wao waliniambia, nilipoliacha maskini kanisa langu la Kibaptisti, kasema, “Utakuwa mtakatifu anayejibingirisha, ukichanganyikana na hao watakatifu wanaojibingirisha.”

¹²⁸ Nikasema, “Sijui wao ni akina nani, lakini kama—kama Mungu ananituma kwao, Yeye ana Ujumbe kwa ajili yao.” Hiyo ni kweli. Kama Mungu akitoa Ujumbe, mtu fulani atausikia mahali fulani. Amina.

¹²⁹ Hivyo ndivyo Yohana alivyowazia wakati alipotoka nyikani, yule Eliya wa Agano Jipya, mtu aliyeparuza, alisema, “Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Alikuwa na hakika na Ujumbe wake, alijua ya kwamba ulikuwa ni wa kweli. Alijua ya kwamba alizaliwa na kumpokea Roho Mtakatifu katika tumbo la mama yake kwa Jina la Yesu Kristo.

¹³⁰ Kwenye umri wa miaka tisa, alienda nyikani bila elimu, akakaa mle mpaka alipokuwa na umri wa miaka thelathini, akatokea bila nguo, amejizungushia tu kipande cha ngozi ya kondoo, naye akahubiri Ujumbe uliotikisa maeneo ya karibu. Amina. Mbona, alikuwa na hakika!

¹³¹ Naye alipomwona Roho Mtakatifu huyo kama Nuru, akishuka pale akiwa na mabawa mawili juu Yake, akishuka juu ya Yesu, alisema, “Sikumjua Yeye, bali Yule aliyenena nami nyikani na kusema, ‘Ambaye utamwona Roho akishuka, na kukaa juu Yake, Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.’ nina hakika nalo.”

¹³² Alipochoka kidogo, kama tulivyozungumzia hivi majuzi usiku, Yesu alisema, “Enendeni, mkamwonyeshe Yohana yaliyotukia.” Iweni na hakika. Iweni na hakika ni sauti inayojulikana.

¹³³ Sasa, Simeoni, alifunuliwa, na Roho Mtakatifu, ya kwamba hataona mauti, na hata hivyo alikuwa ni mzee kwelikweli, hangeona mauti mpaka amwone Kristo wa Bwana. Hakuona haya, alienda huku na huko akimwambia kila mtu, “Sitakufa, nitakuona kuja kwa Kristo.”

¹³⁴ Vema, ninaweza kuwasikia wakisema, “Maskini jamaa mzee, kidogo amevurugika. Anazeeka sasa, mwajua, naye, naamini akili yake inazimika kidogo, mwajua.” Inakufanya ufanye mambo na kutenda kwa njia ambayo hujawahi kutenda hapo awali, wakati unapokuwa na hakika, wakati ukiwa na hakika kabisa.

Simeoni alisema, “La, sitakufa mpaka nitakapomwona Kristo akija.”

¹³⁵ “Sasa,” kasema, “wazieni, Daudi alimtazamia, Musa alimtazamia, na maelfu ya miaka iliyopita walimtazamia. Na sasa sisi hapa katika ninii ya Kirumi...Mbona, angeweza je kamwe kumwona? Maskini huyo jamaa, kamwe msimjali.”

¹³⁶ Hilo halikumsumbua, alienda huku na huku akisema, “Utukufu, sitakufa mpaka nitakapomwona—nitakapomwona Kristo akija, nitamwona.” Siku moja alipokuwa amerudi kwenye

chumba chake cha kusomea huko nje, Yesu aliletwa hekaluni kwa ajili ya tohara, ule utakaso wa Mariamu, amefunikwa nguo za kitoto na—naye akasimama, maskini huyo bikira.

¹³⁷ Nao watu wakajitenga naye kwa sababu kwanza kabisa Yeye alikuwa na jina baya, walisema alizaliwa nje ya ndoa takatifu. Nami ninaweza kuwazia hao wanafiki wa kujifanya, mwajua, kamwe hawakuwa na uhusiano wowote na kitu kama hicho, walibaki katika chumba chao, nyuma. Na, lakini alijua Kile alichokuwa ameshika mikononi mwake, alijua Huyo alikuwa ni Mwana wa Nani.

¹³⁸ Na hivyo ndivyo ninavyosema leo, unaweza kumwita Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili mlokole, ama mtakatifu anayejibingirisha, ama chochote utakacho, kama anajua Huyo ni Roho Mtakatifu, kamwe hutamtikisa. La, bwana. Kamwe hutakuwa na shida naye. Anajua kilichoko mle ndani, anajua kilipotoka.

¹³⁹ Kama nilivyosema daima, dini hii chotara waliyo nayo siku hizi, kama kuna kitu ninachochukia, upuuzi huu chotara wanaozungumzia, *hii* chotara. Nami nafikiri sayansi imefikia mahali wame—wamekanusha hoja yao wenyewe.

¹⁴⁰ Mnajua, wanasema ya kwamba mwanadamu alitokana na, alitoka tu kwa tumbili kisha akapanda juu, na kufikia ninii, kutoka kwa kiluwiluwi na kuendelea, bali Mwanzo 1:26, ilisema, “Kila mbegu na izea kwa jinsi yake.” Ninaamini Mungu aliwaumba tumbili. Naam, bwana. Ninaamini Mungu aliumba kila kitu. Lakini Yeye alimfanya mwanadamu, naye mwanadamu kamwe hakuja kwa mageuzi yenye kuendelea, ati tumbili wakawa wanadamu. Mungu aliumba ndege na vitu vyote hapo mwanzo, na inathibitisha hilo.

¹⁴¹ Ukichanganya chochote na kukichanganyia mbegu, hakiwezi kujizaa tena. Hiyo ni kweli, kimekufa. Wanaendelea mbele, kasema, “Mahindi chotara, mahindi chotara, mahindi mazuri sana.” Ninajua, lakini hayafai kitu, huwezi kuyapanda, hayatarudi tena. Hiyo ni kweli, yamekwisha.

¹⁴² Hebu mchukue nyumbu, nyumbu, nyumbu ndiye jamaa mbaya kuliko wote aliyepo. Mwajua, yeye—yeye—yeye—yeye ni farasi, wala nyumbu, naye—na—na—naye kweli hata hajui yeye ni nini. Hiyo ni kweli. Na mama yake alikuwa farasi jike na baba yake alikuwa punda, kwa hiyo ha—ha—hajui ni wa nani. Naye hawezi kujizaa tena, nyumbu hawezi kumzaa nyumbu, huyo amekwisha. Mnajua hilo.

¹⁴³ Na hivyo ndivyo tu baadhi ya dini hizi zilivyo siku hizi, dini ya nyumbu. Hiyo ni kweli. Unaweza kuzungumza juu ya siku za miujiza, Roho Mtakatifu, na jambo hili lote. Nawe uliwahi kumwona maskini nyumbu? Yeye ni mjinga, anayatokeza tu masikio yake makubwa na kukukazia macho tu. Hana upole wala hisia ya wema. Wala huwezi kumtumia kwa lolote,

atangojea maishani mwake mwote akupige teke, kisha angoje mpaka ufe, ndipo wakati akifa, atakupiga teke.

Naye atasimama pale na hayo masikio makubwa, aseme, “Njoo, jamani. *Whiu, whiu, whiu.*”

Yeye tu ni, “Hoo, hoo!” Mnaona, yeye hajui chochote, yeye ni chotara.

¹⁴⁴ Hiyo ndiyo shida ya baadhi ya dini hii chotara. Unaweza kusema, “Yesu Kristo ni yeye yule, jana na hata milele.”

¹⁴⁵ Wanapiga makelele, “*Hoo, hoo!* Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama hicho.” Loo, jamani! Si ajabu Biblia ilisema wangukuja kama uwanja wa nyumbu wanaolia. Hiyo ni kweli. Loo, ni, hiyo ni kweli, ni chotara. Ulijaribu kufanya nini? Kuchanganya baadhi ya ulimwengu na Kanisa. Hilo ndilo lililoanza hapo mwanzo, kanisa chotara. Hatuninii . . . sisi ni . . .

¹⁴⁶ Lakini mnajua kitu kimoja ambacho ni kipole, kitu kimoja ninachopenda ni farasi mzuri, ukoo safi. Loo, jamani! Huyo farasi ukoo safi anaweza kukwambia baba yake alikuwa ni nani, mama alikuwa ni nani, babu yake alikuwa nani, nyanya, mama wa nyanya, wa nyanya, wa nyanya, wa nyanya, wa nyanya, wa nyanya, kurudi nyuma, yeye ni ukoo safi. Hivyo ndivyo ninavyopenda kumwona Mkristo ukoo safi, amina, mtu anayejua baba yake ni nani na mama yake ni nani.

Ukisema, “Je, wewe ni Mkristo?”

¹⁴⁷ “Mimi ni Mmethodisti.” Vema, hayo ni maungamo mazuri ya kwamba wewe si Mkristo. “Mimi ni Mbaptisti.” “Mimi ni Mpresbiteri.” “Mimi ni Mpentekoste.” Ndugu, sisi ni Wakristo kwa sababu sisi ni ukoo safi, tumezaliwa kwa Roho Mtakatifu. Ninajua Baba yangu ni Nani. Amina.

¹⁴⁸ Mkristo ni Mkristo! Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” Mkristo ukoo safi, yule aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Hakuna sauti isiyojulikana kuhusu hilo. La, bwana. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyosikika kwenye Siku ya Pentekoste, kwa hiyo ingali inasikika vile vile. Na ni sauti halisi, inayojulikana. Hiyo ni kweli. Hiyo ni sauti moja nzuri, inayojulikana. Naam.

¹⁴⁹ Simeoni, alikuwa na hakika atamwona.

¹⁵⁰ Yesu alikuwa na hakika na Neno la Baba. Mbona, bila shaka. Wakati Mariamu alipokuja pale, na—naye akasema, ama Martha, hasa, akasema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu hangalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atafanya.”

¹⁵¹ Naye akasema, “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniadini Mimi hatakufa kamwe. Je, unasadiki haya?”

Akasema, “Naam, Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, sawasawa na usemavyo. Ninaamini Wewe ndiwe yule Masihi aliyekuwa aje ulimwenguni.”

Kasema, “Mmemzika wapi?”

¹⁵² Sasa, Yeye hakusema, “Ni—nitashuka niende nione kile ninachoweza kufanya juu yake.” Loo, la. “Nitaenda kumwamsha.” Sio, “Nitaenda kujaribu.” “Nitamwamsha!” Amina. Hilo ni hakika. Yesu alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha, hiyo ni Yohana Mtakatifu 5:19, “Sifanyi neno lolote mpaka nimwone Baba akilitenda, anionyeshe Mimi kwanza.” Naye Baba alikuwa amemwonyesha ya kwamba Lazaro alikuwa anaenda kufufuka katika wafu, kwa hiyo kabla ya neno lolote kusemwa, Yeye alisema, “Nitaenda nikamwamshe.” Sio, “Nione kama ninaweza.”

¹⁵³ Akasema, “Nina uwezo wa kuutoa uhai Wangu, na kuutwaa tena.” Hakuna mashaka juu ya hilo, hakuna jambo lisilo na hakika kuhusu hilo. “Mkiniua, iharibuni maskani hii nami nitaijenga tena katika siku tatu.” “Iharibuni hii, nitaijenga!” “Ati nitajaribu nione kitakachotukia?” “Nitaijenga!” Kwa sababu Daudi alisema, “Sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Alijua katika saa sabini na mbili uharibifu utaingia, na mahali fulani, kabla ya hizo saa sabini na mbili kwisha, mwili wa Yesu ulikuwa unaenda kufufuka kutoka kwa wafu. Hakuna mashaka juu yake, Yeye alilitumainia Neno la Mungu kwa dhati. Amina. Kila kitu alichofanya, alitumainia Mungu kwake.

¹⁵⁴ Sasa, Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya.” Hakuna mashaka juu ya hilo, Yeye alisema kwamba ilikuwa ni hakika, “Yeye atafanya.” Alilipa Kanisa Lake agizo, kasema, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kwa Jina Langu *watatoa* pepo, *watanena* kwa lugha mpya. Wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, *watapata* afya.” Hakuna kitu kisicho na hakika kuhusu hilo. Hiyo ni kweli.

¹⁵⁵ Yesu alisema, “Katika siku za mwisho,” ama, Roho alisema, Biblia, ilisema, “watu watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasingizaji, wasiojizua, na wasiowapenda walio wema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wenye mfano wa utauwa na wangezikana nguvu zake.” Hakuna mashaka juu yake, tunao. Amina.

¹⁵⁶ Danieli alisema watu waliomjua Mungu wao katika siku hizi wangetenda mambo makuu. Hakuna jambo lisilo hakika kuhusu hilo, Mungu alisema hivyo, tunalo. Amina. Hakuna kitu kisicho na hakika juu yake.

Loo, mtu fulani alisema, “Ndugu, Roho Mtakatifu alikuwa kwa ajili ya jambo hilo, kwa ajili ya Wapentekoste huko nyuma.”

¹⁵⁷ Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hakuna mashaka juu ya hilo, watalipokea. Hiyo ni kweli, watafanya hivyo. Kila mmoja, wote watakaoitwa na Bwana Mungu, mbona, Yeye atawapa Roho Mtakatifu. Maadamu watafuata tu maagizo, hilo tu ndilo wanalopaswa kufanya, hakuna mashaka kulihusu, la.

¹⁵⁸ Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu,” jinsi Malaika wa Bwana angeshuka, na, miongoni mwa watu na kuonyesha ishara hizi na maajabu, maajabu ya kufufuka Kwake. Ametoka, amefufuka kutoka kaburini miaka elfu mbili, ulimwengu hauamini hilo. Lakini Yeye... “Kwa kuwa Yeye yu hai,” Yeye alisema, “sisi nasi tunaweza kuishi.” Hakuna mashaka juu yake.

¹⁵⁹ Kazi alizofanya Yeye, sisi pia tunaweza kuzifanya, hakuna mashaka juu yake, ahadi Zake zote ni, “Ndiyo,” kwetu. Tunaishi katika siku za mwisho, tunaona kila kitu jinsi hasa Yeye alivyosema, kwa hiyo hakuna mashaka. Unaweza kuliadini, weka tumaini lako ndani yake.

¹⁶⁰ Paul Rader, wengi wenu nyote mnamkumbuka, kutoka Chicago hapa, mtu mashuhuri wa Mungu, alikufa hapa miaka michache iliyopita. Daima nimempenda Paulo. Nami nilimsikia mara chache nilipokuwa mvulana. Ndipo nikaketi kwenye Maskani ya Rediger pale, kwenye chumba alimoandikia ule wimbo, *Amini Tu*, ambao umeniongoza mimbarani kwa mamia ya lugha mbalimbali, nadhani, kote ulimwenguni, *Amini Tu*. Nami nashangaa kama Paul alijua ya kwamba maskini jamaa huyo mdogo, aliyeketi pale nje amevaa ovaroli, angechukua wimbo na kuupeleka kote ulimwenguni, ule aliokuwa akiandika.

¹⁶¹ Nilikuwa nimeketi pale, nikiwa na mkutano hapa wakati fulani uliopita, na huo ukaingia kupitia maikrofoni, nilipiga tu magoti na kulia, kwa sababu nikijua ya kwamba alikuwa ni mtu mashuhuri sana wa Mungu.

¹⁶² Alikuwa akisimulia hadithi wakati mmoja katika kitabu chake, nilikuwa nikiisoma. Nafikiri alitoka Oregon, naye alikuwa akikata miti, alikuwa mtu mwenye nguvu. Luke alikuwa mtu mwenye nguvu sana, ndugu yake. Na kwa hiyo, Paul akasema yeye, huko, huko kwenye, ninaamini ilikuwa ni nchi ya kigeni alimokuwa, alikuwa, alishikwa na homa ya maji meusi, ama chochote kile, alikuwa—alikuwa yuafa.

163 Naye akamwambia mke wake mwaminifu asimame karibu naye, maana wasingeweza kumleta daktari mle ndani, ilikuwa ni huko nyuma sana. Ndipo giza likazidi kuingia chumbani, naye akasema, “Mpenzi,” akasema, “simama karibu nami, endelea tu kuomba, endelea kuomba.” Paul alikuwa mwaminio mashuhuri katika uponyaji wa Kiungu. Na kwa hiyo, alihubiri papa hapa katika mji huu hapa chini maskanini. Na kwa hiyo, aliamini jambo hilo, alimfanya mke wake aendelee kuomba. Kwa hiyo haidhuru itakuwaje, endelea tu kuomba.

164 Alisema ikawa giza zaidi na zaidi chumbani, na hatimaye kila kitu kikaingia giza. Naye akasema alikuwa akiota, alidhani alikuwa amerudi Oregon tena. Naye alikuwa. . . Bosi alimwambia, wa hiyo kambi ya miti ambapo alikuwa akifanya kazi, kasema, “Paul, panda kule kilimani unikatie mti fulani, ukubwa fulani, na kuuleta hapa chini.”

165 Akasema, “Vema.” Kasema alikimbia juu kilimani, naye angeweza kunusa harufu ya msonobari, huku mapafu yake yakiinusia, mwajua, hiyo harufu, jinsi mtu anayeishi mwituni anavyoweza tu kufurahia. Naye akasema aliukata huo mti, na kuupogoa, akalichomeka shoka ndani yake, akaushika huo mti wala asingeweza kuuinua. Kasema aliweka magoti yake pamoja na kuinamisha mgongo wake, sehemu yenye nguvu sana ya mtu iko kwenye mgongo wake na misuli, angeinua na kuinua. Naye akasema, mbona, angeweza kuinua mti mara mbili ya ukubwa huo, lakini kwa namna fulani, aling’ang’ana nao, na kung’ang’ana nao, na kung’ang’ana nao, na kwa kweli asingeweza kufanya chochote nao.

166 Hivyo ndivyo watu wengi wafanyavyo, wananinii tu, wanachukua Neno, nao wanajaribu kuliendesha *hapa* na kuliingiza *hapa*, ama kulifanya *pale*, na kushindana Nalo, na kushindana Nalo, kulipitisha katika seminari, na kulikatia *hapa* chini, na kufanya neno la Kiyunani kutoka Kwake *hapa* na neno la Kiebrania kutoka Kwake *hapa*, na muda si muda mwajua, inakuwa *hivyo*, wala hakuna Neno la Mungu. Mnaona? Unang’ang’ana tu Nalo na kung’ang’ana Nalo.

167 Unalipeleka kwa Dk., Ph.D. John Doe, na kumwuliza anachowazia juu Yake. Na kwa Ph.D. Sam Doe, na kumwuliza la kuwazia juu Yake, naye akasema, “Mbona, ni telepathia ya kiakili.” Huyu mwingine akasema, “Ni ulokole.” Na jambo la kwanza, unashindana tu Nalo na kung’ang’ana Nalo.

“Vema, nilikuwa huko chini mkutanoni na—na kwa kweli, nikamwona Roho wa Mungu akishuka. Nilimsikia mtu fulani akinena kwa lugha zisizojulikana.”

“Ni ibilisi.”

“Naam, kisha nikasikia watu wakipaza sauti.”

“Loo, ni msisimko.”

168 “Ndipo nikamwona mtu akisimama jukwaani, na kwa nguvu za upambanuzi akawaambia watu wao ni akina nani, na huko nje mikutanoni, na kuna shida gani. Na jinsi tu Biblia ilivyosema Yesu alilifanya, kuonyesha ishara ya Masihi.”

“Vema, nitaenda nimwulize mchungaji wangu.”

Akasema, “Ah, ni telepathia.” Mnaona? Unaendelea tu kung’ang’ana Nalo na kung’ang’ana Nalo. Hivyo tu. Kamwe hutafika popote.

169 Hatimaye, Paul akasema alikuwa amechoka, kwa hiyo akaketi chini, nguvu zake zilikuwa zimeisha. Aliketi tu chini akaegemea mtini na kuegemea nyuma, kasema, “Kwani nguvu zangu zimekuwaje?” Bila shaka hiyo ilikuwa ni homa iliyomshika, ilikuwa ikifanya hivyo. Naye akasema, “Ni—niko tu mwisho.”

Kasema baada ya kitambo kidogo akasikia Sauti tamu sana, kasema, “Paul?”

Akasema, “Huyo ni boshi wangu?” Naye akasema alipogeuka, kweli ilikuwa ni Boshi wake, kasema hajawahi kuona uso mzuri zaidi maishani mwake mwote.

Akasema, “Paul, kwa nini unang’ang’ana nao?” Akasema, “Unaona kile kijito cha maji pale?”

Kasema, “Naam.”

170 Kasema, “Kijito hicho cha maji kinashuka moja kwa moja kukizunguka hiki kilima hapa, nacho huja moja kwa moja kambini.” Kasema, “Kwa nini usiutupe tu majini, halafu uupande uteremke chini?”

“Loo,” akasema, “Kamwe sikuwazia hilo.”

171 Kwa hiyo akautupa tu majini, akaanza kuteremka juu ya mawimbi, akipiga mayowe kwa sauti yake yote, “Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!” Naye akasema alipojirudia, alikuwa amesimama katikati ya sakafu, akipiga mayowe, kwa sauti yake yote, “Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!” ahadi ya Mungu.

172 Basi usiku wa leo, ndugu, hakuna mashaka kuhusu Neno la Mungu, nimepanda juu Yake. Litanifikisha Kambini siku moja. Sijui itanibidi kuvuka mawimbi mangapi, lakini nimepanda juu yake. Amina. Mungu asifiwe.

173 Hebu sote tuliseme pamoja: “Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!” Ni ahadi ya Mungu. Nimepanda juu yake! Ni sauti ya hakika, ni sauti ya Mungu, ni Sauti Yake. “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Nami nimepanda juu Yake usiku wa leo. Yeye aliahidi mambo haya katika siku za mwisho, nami ninaamini yapo hapa.

174 Hebu waliite chochote watakacho, sijali, hilo halijalishi kwangu, nina hakika kwamba ni Mungu. Amina. Nami

nimepanda juu yake! Nimekuwa nikilipanda sasa kwa miaka thelathini na mmoja, na safari inazidi kuwa tamu wakati wote, kwa sababu nimekaribia langoni. Amina. Ningali nimepanda juu yake.

¹⁷⁵ Mauti yanapoupiga mwili wangu, nitapanda juu yake, niendeleo tu kupanda. “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima,” asema Mungu, “yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe.” Nimepanda juu yake, sina mashaka kuhusu hilo, nimepanda juu yake. Nalo ni Neno Lake, nami ninaliamini kwa moyo wangu wote. Mnaliamini vivyo hivyo? Kitu kingine chochote hakina hakika, lakini hiyo ni sauti ya inayojulikana, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya.”

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa hivi.

¹⁷⁶ Kuna kila namna ya sauti zisizojulikana: haijulikani kwamba mji huu utakuwa umesimama mnamo asubuhi, sijui; hakuna hakika kwamba utawahi kufika nyumbani usiku wa leo, sijui; hakuna uhakika kwamba nitawahi kuwa Chicago tena, sijui; hakuna uhakika kwamba tutakutana tena, sijui. Mnaona? Ila kuna Jambo moja ambalo ni la hakika, hilo ni Neno la Mungu.

¹⁷⁷ Sijui ni, muda gani zaidi tutaninii... muda gani zaidi tutakuwa taifa, itachukua muda gani kabla hatujalipuliwa vipande-vipande, sijui, haijulikani. Lakini kuna Jambo moja ambalo ni la hakika, hilo ni Neno la Mungu. Nimepanda juu yake, enyi marafiki, ninaliamini kwa moyo wangu wote, kwa nafsi yangu yote. Nimepanda juu Yake.

¹⁷⁸ Nanii wetu wa Mbinguni. . .

[Ndugu mmoja ananena kwa lugha na ndugu mwingine anafasiri—Mh.]

¹⁷⁹ Ee Bwana, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hilo! Sasa, Baba Mungu, hili, hatutakuwa na udhuru wa kusikia sasa, isitoshe, bali kusikia unabii Wako, kuwasikia wakinena katika unabii na kuona yakitimizwa, kuona ahadi za Mungu, za kufufuka, za kuhuishwa, za kuja tena, na ile ishara kuu ya Masihi ya Yesu aliyefufuka kuonekana mbele ya Mataifa, kama ilivyowafanyia Wayahudi na Wasamaria, katika siku hizi za mwisho.

¹⁸⁰ Ee Baba Mungu, tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili, ninakushukuru. Sasa, hayo maneno Mungu, yakitoka Kwako, bila shaka, baada ya mimi kujaribu kuyaleta katika Biblia, na kukusikia Wewe ukilinena kupitia karama za lugha na tafsiri, sasa, tunaomba ya kwamba utamruhusu Yesu aje miongoni mwetu na kuthibitisha hili kuwa ni kweli, kusudi kila mtu aweze kuwa na majaliwa ya kujua ya kwamba Yesu yeye yule, aliyekuwa wakati mmoja pamoja na wana wa Israeli, katika Wingu, ambalo liliitwa Ubaba, pia alikaa miongoni mwa wanadamu katika Uwana, na sasa anakaa ndani ya mwanadamu

kwa Roho Mtakatifu, Baba, jalia waone ya kwamba tabia ile ile ya Mungu inabaki vile vile, iliyokuwa ndani ya Yesu, ndivyo ilivyo katika Kanisa, na kufanya kazi zile zile hapa katika siku za mwisho, ambapo Kanisa limefikia hatima yake.

¹⁸¹ Na sasa ishara ya Masihi ya wakati wa mwisho, maangamizi yako tayari, kama ilivyokuwa kwa Wayahudi katika siku hizo, iliwabidi kumkana Masihi huyo kusudi maangamizi yaje. Na siku hizi mataifa wanacheka, wanaidhiki, na kuiita kila jina chafu. Basi ulipofanya hivyo, ulipokuwa hapa, wao walisema, “Tlikuwa ni Beelzebuli, ibilisi.” Nawe ulisema utawasamehe, lakini siku moja Roho Mtakatifu atakapokuja, kusema neno moja dhidi Yake isingesameheka.

¹⁸² Na sasa, Baba, tunaona ya kwamba mataifa yamejihukumu yenyewe, maneno yao, katika matendo yao. Makanisa, watu wengi, wengi sana wamehukumu, na kutia sahihi maangamizi yao wenyewe, kumwita Roho wa Mungu kitu kichafu.

¹⁸³ Sasa, hii ni nafasi nyingine, usiku wa leo. Ninaomba, Baba, ya kwamba utamponya kila mgonjwa hapa, uokoe kila asiyeokoka, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

[Dada mmoja ananena kwa lugha na ndugu mmoja anafasiri—Mh.]

¹⁸⁴ Amina. Mungu ashukuriwe. Sasa, kulingana na hilo Yeye ameahidi kuwa hapa. Sikuwa ninaenda kufanya . . . Nilikuwa tu ninataka kufanya wito wa madhabahuni, lakini ninaamini sasa, ninahisi upako wa Roho kwa ajili ya jambo lingine.

¹⁸⁵ Kamwe hatukusambaza kadi zozote za maombi leo, mnaona, kwa hiyo hatuna kadi za maombi, bali tunaye Kristo. Ni wangapi walio wagonjwa huko nje na wanataka kuponywa? Inueni mikono yenu popote mlipo. (Asante, mlinzi.) Sasa, ambapo . . . Kama nimehubiri kweli za kweli na kufanya jambo lililo sahihi, basi Mungu anawajibika kuunga mkono yale niliyosema. Sasa, ni wangapi wenu huko nje mnaojua ya kwamba siwajui, inueni mikono yenu, kwamba siwajui. Kila mahali.

¹⁸⁶ Ninyi Wapentekoste, je, inapaswa kuwa ni vigumu kwenu kuniamini mimi? Angalieni hapa, ninataka kuwaonyesheni jambo fulani hapa, lililoandikwa hivi majuzi tu. Nilikuwa kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara Wakristo huko California, nami ndiyo kwanza nimalize kuhubiri mahubiri ambayo nilifikiri nilirarua kila dhehebu na kulianika vipande-vipande. Ndipo mvulana wa Kibaptisti jina lake Danny Henry, akaja kunikumbatia kwa mikono yake aombe, ndipo akaanza kunena kwa lugha zisizojulikana. Basi kulikuwa na mama aliyeketi huko nje kutoka Louisiana, mama Mfaransa, akasema, “Hiyo haihitaji fasiri yoyote,” kasema, “hiyo haikuwa ni lugha zisizojulikana, yeye aliongea Kifaransa.”

¹⁸⁷ Mtu mwingine akasema, “Kifaransa.” Ndipo ikatokea akashuka akaja, wakayakusanya pamoja, tunayo hapa, na kila

mmoja alikuwa akitoa tafsiri. Naye mkalimani wa UN alikuwa pale, naye akasimama, akasema, akashuka. Mtu alisema hapa, hajawahi kumwona hapo kabla wala baadaye, bali yeye alikuwa, alitaja jina lake, kwamba alikuwa nani, mkalimani wa UN, naye akatoa tafsiri. Nimeyaandika hapa. Sikilizeni hapa, huenda mkafikiri mimi ni mgumu, angalieni hapa:

Kwa sababu umechagua njia iliyo nyembamba, njia iliyo ngumu zaidi, umetembea kwa chaguo lako mwenyewe.

Sasa, ninaweza kuelewa hilo. Ilimbidi Musa atembea kwa chaguo lake mwenyewe, haikumbidi kutembea, bali a—alifanya uamuzi wake. Huo ulikuwa uamuzi wangu kudumu na Neno, haidhuru lilifanya nini. Mnaona? Ninaweza kuona. . .

Umefanya hivi kwa chaguo lako mwenyewe. Umechagua uamuzi sahihi na dhahiri, na ndiyo NJIA YANGU. (Asante Mungu!) Kwa sababu ya uamuzi huu muhimu sana, sehemu kubwa ya Mbingu inakungojea.

Sasa, mtu huyu kamwe hakujua lolote kuhusu ono hili, maana nililipata tu siku chache kabla ya hapo, mnaona.

Ni uamuzi mtukufu jinsi gani uliofanya! Hili, lenyewe, ndilo litakalotoa, na kufanya utimie, ule ushindi mkuu sana katika Upendo wa Kiungu.

¹⁸⁸ Hilo lilitafsiriwa na mkalimani wa UN, na mvulana Mbaptisti aliyekuja kunikumbatia kwa mikono yake, kisha akatoa tamshi tu, kasema, “Ujumbe huo kweli ungeweza kuongezwa kwenye Kitabu cha Ufunuo.” Mnaona? Mvulana ambaye ha—hakunijua mimi. Yeye ana uhusiano fulani na nyota fulani wa sinema kule. Na yeye—yeye kamwe hakunijua, mvulana wa Kibaptisti, naye a—alikuja tu ku—kunishukuru, na kunikumbatia kwa mkono wake kuomba, ndipo alipofanya hivyo, Roho Mtakatifu akaanza kunena kwa lugha kupitia kwake. Na hawa hapa watu wameketi pale kama tu ilivyokuwa kwenye Pentekoste. Ilikuwa—ilikuwa ni lugha waliyoelewa, hiyo ilikuwa ni lugha yao ya mama, naye mvulana huyo hakujua hata neno moja la—la Kifaransa. Mnaona jinsi ilivyo? Ni Roho Mtakatifu. Amina.

¹⁸⁹ Yuko hapa. Vema, ombeni sasa. Niliwaambia katika Biblia yule Malaika aligeuza mgongo Wake kuelekea kwenye kusanyiko. Mtu fulani katika sehemu hizi hapa, mtu fulani katika sehemu hizi hapa ndani, wewe mwombe Mungu akutendee jambo fulani, uone tu kama Yeye angali ni Malaika yule yule wa Mungu, ama mtu fulani mahali popote, popote pale.

¹⁹⁰ Nitaangalia kwenu ninyi ndugu, ninawatakeni mwamini, ndugu. Huyu ndiye Kristo ambaye mmemhubiri kwa muda mrefu sana, hili ndilo jambo ambalo mmelitetea. Ninyi wanaume, kukiweko na heshima yoyote ya kutolewa, ni kwenu nyote, mlikuwa hapa nje, Wapentekoste, mkihubiri, huku nje

pembeni mwa barabara mkiwa na tari na magitaa, walipokuwa wakicheka, wakiwadhihaki, mlikuwa tu mkitengeneza barabara ambayo ningeweza kuipitia vizuri. Ningewezaje kuja na kuwa kitu kingine chochote ila ndugu yenu? Mlitabiri ya kwamba mambo haya yangekuja, wengi wenu, mliyasikia katika mikutano yenu. Nami nipo tu hapa katika kutimiza yale mliyosema kwamba Neno la Mungu linasema. Mnaona?

¹⁹¹ Sasa, mtu fulani anawasiliana na Mungu, huku nyuma. Kuna mtu aliyeketi nyuma yangu, mahali fulani nyuma huku, anaomba, ana tatizo ubavuni mwake. Ana ugonjwa wa wasiwasi unaomsumbua. (Kuna mtu aliyesimama? Hakuna aliyesimama?) Ninamwangalia mtu huyu papa hapa. Mtu huyo ni mhudumu. Yeye ni Mmenoni. Jina lake ni Bw., Kasisi Miller. Simama, ukubali uponyaji wako. Hatufahamiani, bwana. Sikujui wewe. Loo, je, yale yaliyosemwa, hayo yalikuwa ni kweli? Kama ni kweli, waweza kusimama tena? Vema.

Mnaamini? Sasa, Yesu alisema nini? Mambo haya yangetukia.

Malaika yule yule wa Mungu aliyesimama karibu na Ibrahimu na kusema, “Yu wapi Sara, mkeo?”

Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

Naye akasema, “Nitakuzuru kulingana na muhula wa uhai.”

¹⁹² Naye Sara, kama nilivyowaambia Jumapili iliyopita, ya kwamba uhusiano wa kifamilia haukuwapo kwa miaka mingi, akasema, “Ati mimi nipate raha na bwana wangu tena, huko nje, akiwa ni mzee nami mkongwe? Haiwezekani.” Naye akacheka.

Ndipo yule Malaika akasema, “Kwa nini akacheka, akisema ya kwamba mambo haya hayawezekani?”

Alisema lingekuwa ni jambo lile lile wakati wa mwisho. Iweni na imani, aminini.

¹⁹³ Huyu mama mweusi aliyeketi papo hapo nyuma, shida ya kike, ameketi mwishoni mwa safu. Naam, mama. Je, una kadi ya maombi? Huhitaji yoyote. Huna yoyote, huhitaji. Je, una shida ya kike? Hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Hivi hukuwa ukiomba wakati huo, “Bwana, jalia iwe ni mimi, usiku wa leo?” Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako *hivi*. Vema. Umepata shauku yako, nenda nyumbani, Yesu Kristo amekuponya.

Kama unaweza kuamini! Aminini tu.

¹⁹⁴ Mtu huyu aliyeketi hapa, wa pili kutoka mwisho, akija mle, papa hapa, uligeuza kichwa chako na kuangalia, matatizo na shida ya mapafu na kadhalika. Unaamini ya kwamba Kristo atakuponya?

¹⁹⁵ Jamaa mkubwa mwishoni, mtu wa pili nyuma, akiingia. Unaamini kwa ninii yako yote...? Naam, bwana, ni wewe. Papa hapa, mtu huyo mwingine papa hapa, bwana. Simama

kwa miguu yako. Huyu ndiye mtu hapa ambaye Nuru hiyo iko juu yake. Vema, pokea uponyaji wako. Nenda nyumbani ukaamini. Amina. Hatufahamiani, sikujui wewe. Si—sikujui, hatufahamiani. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁶ Mwanamke huyu aliyeketi papo hapo karibu na huyo mwanamume aliyesimama hapo, unataka kupona hicho kisukari? Na kuamini kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu atakuponya? Kama utaamini, simama, useme, “Amina.” Vema. Huyu ni Yeye.

Unaweza kupokea uponyaji wako kama unaamini. Lakini huna budi kuamini, sivyo?

¹⁹⁷ Mama huyu, naam, unayepunga mkono wako, uliyeketi huko nyuma kwenye kusanyiko, unaamini uvimbe huo utakoma, binti yako pale aliye na kifafa atakoma kuwa nacho tena? Bibi Smallwood, unaweza kwenda nyumbani sasa, na kila kitu ni sawa. Unaweza kuponywa, kama utaamini kwa moyo wako wote. Hatufahamiani, sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu. Kama ndivyo ilivyo, inueni mikono yenu, nyote wawili. Inueni tu mikono yenu hapo. Hiyo ni kweli kabisa.

Unaamini kwa moyo wako wote? Vipi kuhusu baadhi yenu watu mnaoketi hapa chini? Unaninii, amini kwa moyo wako wote? Basi amini.

¹⁹⁸ Vipi kuhusu wewe uliyeketi hapa, huyu mtu mweusi aliyeketi hapa akiniangalia. Una kadi ya maombi? La. Huhitaji yoyote, unayo imani, na hiyo tu ndiyo unayohitaji. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Hatufahamiani. Sisi ni jamii mbili mbalimbali za watu, na mara yetu ya kwanza kukutana. Lakini unaonekana una hisia nzuri kwa roho yako, una imani ya namna fulani. Hiyo ni imani nzuri kwa mtu mwingine unayemwomba hata hivyo. Hiyo ni kweli. Dada yako, ana kansa. Hiyo ni—hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Vema, amini naye atapona.

Unaamini kwa moyo wako wote? “Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana.”

¹⁹⁹ Bibi Johnson, unataka kwenda nyumbani na uwe mzima pia? Unaamini kwa moyo wako wote? Jackson, hasa, nilimaanisha kusema. Kama utaamini kwa moyo wako wote, nenda nyumbani, uwe mzima pia.

²⁰⁰ Vipi kuhusu mwanamke huyu aliyeketi hapa? Ninii... Unaamini kwa...? Naam. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Una shida kwa miguu yako, shida kwa mikono yako. Unamwomba mtoto, ugonjwa wa akili. Kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kupata kile unachoomba. Unaamini? Usilie, shukuru tu.

201 Ni wangapi wa wengine wenu wanaoamini? Unaamini kwa moyo wako wote? Ni wangapi wanaomwamini Yeye kama Mwokozi wenu sasa? Hiyo si sauti isiyojulikana. Biblia inasema, Hiyo ni sauti inayojulikana, “Ishara hizi zitafuatana na hao. Katika siku za mwisho itatukia.”

202 Ninyi mnaotaka kumpokea kama Mwokozi, kama mko hapa, simameni kwa ajili ya ushahidi, useme, “Nitampokea kama Mwokozi wangu,” wakati mkiwa katika Uwepo Wake. Wakati upako wa Roho Mtakatifu ukiwa juu ya watu, waweza kumpokea kama Mwokozi? Simama kwa miguu yako, kama uko hapa, mtu fulani anayemhitaji kama Mwokozi.

203 Ni wangapi hapa ambao hawajampokea Roho Mtakatifu? Mungu akubariki, Dada. Mtu fulani hapa, ambaye hajampokea Roho Mtakatifu, simama kwa miguu yako, useme, “Nitampokea, naam, hakika. Nipe Roho Mtakatifu usiku wa leo.” Mnaamini? Simameni.

204 Mbona, Yeye yupo hapa, ni Roho Mtakatifu Mwenyewe. Endeleeni tu kusimama, endeleeni kusimama, endeleeni tu kusimama kwa miguu yenu. Wote wanaotaka ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao hawajampokea, amini unaweza kumpokea usiku wa leo, simama kwa miguu yako, umpokee tu. Vema. Hakuna sauti isiyojulikana kuhusu hilo sasa.

205 Kumbukeni, “Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watajazwa,” hakuna lisilo hakika. Mnaamini? Basi utajazwa. Kama imani yako ni ya kweli, huna budi kujazwa.

206 Angalia hapa, kwa nini ulilete. . . ? Angalieni hapa mahali panaponibidi kusimama. Sina budi kusimama hapa kabla, loo, kila kitu, na haina budi kuwa *hivyo*, amina, haina budi tu kuwa *hivyo*.

207 Sasa, ni wangapi wenu walio wagonjwa na wanataka kuponywa? Simameni kwa miguu yenu, mwamini mtaponywa, usiku wa leo. Kama huamini, usisimame. Lakini kama unaamini, nawe ulihisi sa—sauti fulani ikiupiga moyo wako, “Hii ndiyo saa nitakayopata uponyaji wangu, hii itakuwa *ndiyo*, sasa hivi.” Kama unaamini kwa moyo wako wote, simama tu kwa miguu yako. Jambo ndilo hilo. Hebu—hebu mwache tu Roho Mtakatifu atende kazi moja kwa moja moyoni mwako nawe utaona jambo fulani likitukia.

208 Sasa, kweli unaamini, kile ulichosimamia, utakipata? Basi inueni mikono yenu na kusema, “Asante, Bwana Yesu. Sasa ninapokea uponyaji wangu. Sasa ninapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Mpeni tu sifa. Amina. Mungu asifiwe. (*Nitamsifu.*)

209 Hiyo ni kweli. Kaeni papo hapo. Msi—msininii. . . Wekeni tu mikono yenu. . . (Nimekwisha kuwaombea. . . ? . . .) Si ni ajabu? Mnauhisi Uwepo Wake? Laiti mngalisimama hapa, mwangalie kile ninachoangalia. (Hilo linaonekana zuri. . . ? . . .) Amina. Vema.


Nitamsifu, nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenye dhambi;
 Mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

²¹⁰ Mnampenda? Mnaamini mmeponywa? Semeni, “Amina. Sasa ninaudai. Nimepanda juu yake. Nimepanda juu yake. Mungu aliihidi, nimepanda juu yake, ninaamini kila Neno lake.” Basi hebu tuinue mikono yetu na kuuimba tena.

Nitamsifu, nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenye dhambi;
 Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwa kuwa Damu Yake imeosha . . .

²¹¹ Siamini mngefikiri ningekuwa mnafiki, ama mwongo. Laiti mngaliweza tu kuele- . . . afadhali ni—nisiseme. Lakini sikilizeni hapa, enyi marafiki, kama vile tu upako, kama tu ninii, kama hiyo—hiyo Nuru ninayoiangalia, inazunguka tu kila mahali. Loo, jamani! Utukufu! Kama ukijiweka tu wazi!

Nitamsifu, nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenye dhambi;
 Mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwa kuwa Damu Yake imeosha . . .

Mungu awabariki. 

61-0429E Sauti Isiyojulikana
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org